**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Arobaini na Saba – Tarehe 17 Agosti, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samwel J. Sitta) Alisoma Dua*

**KIAPO CHA UAMINIFU**

Mjumbe afuataye aliapa Kiapo cha Uaminifu na kukaa katika nafasi yake Bungeni:-

Mheshimiwa Dr. Christina G. Ishengoma.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Christina Gabriel Ishengoma, ndiye aliyechukua nafasi ya Viti Maalum iliyoachwa wazi na Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):**

Taarifa ya 42 ya Mwaka na Hesabu za Shirika la Bima la Taifa Tanzania kwa Mwaka 2005 *(The 42nd Annual Report and Accounts of The National Insurance Corporation of Tanzania Limited for the Year, 2005).*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Taarifa ya Uchapishaji wa Tangazo la Serikali Na. 121 Kuhusu Kuondolewa kwa Sheria Zilizofutwa na Kuzipatia Sura Mpya Sheria Mbalimbali kwa Mwaka 2007 *(The Laws Revision (Replacement of Repealed Laws and Assignment of New Chapters) Notice, 2007).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 430

**Taa za Barabarani – Mji wa Moshi**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Moshi ni kati ya Miji misafi Tanzania lakini unagubikwa na tatizo la giza usiku kwa kukosekana kwa taa za barabarani; na kwa kuwa tatizo hili ni sugu karibu katika Miji yote nchini hata Dar es Salaam ambao ni kioo cha nchi: Je, Serikali ina mikakati ipi ya kuhakikisha kuwa Miji yetu inawekewa taa zinazowaka ili pia kuzuia vitendo vya kihuni na vya ujambazi nyakati za usiku?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa na Mamlaka za Miji ya Mwaka 1982, kifungu cha 62(h), kipengele cha 74 cha jedwali, Halmashauri za Miji zina wajibu wa kuhakikisha kwamba, Miji yetu inawekewa taa *(Street Lights)*. Kama ilivyokuwa kwa Miji mingi ya zamani nchini, mitaa mingi ya katikati ya Miji ilikuwa imewekewa taa za barabarani, lakini kwa muda mrefu zimekuwa hazifanyi kazi. Hii ni kutokana na sababu mbalimbali, zikiwemo kupanda kwa gharama za matengenezo na uendeshaji. Hata hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa taa za barabarani, tayari Halmashauri za Miji zimeanza kuchukua hatua za kurejesha huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, taa za barabarani zina umuhimu mkubwa kwa wakazi wa Miji yetu, ikiwa ni pamoja na kuzuia vitendo vya kihuni na ujambazi nyakati za usiku. Hata hivyo, ni vigumu kueneza huduma hiyo kwa maeneo yote ya Miji hivyo, vipaumbele huwekwa katika maeneo yenye misongamano ya watu na shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi ambazo hufanyika usiku. Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri, imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuhakikisha kwamba, Miji yetu inawekewa taa zinazowaka. Mifano michache ni kama ifuatavyo:-

- Katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi, taa zinazowaka ni 65 kati ya taa 395 zinazohitajika (sawa na asilimia 16.4 ya taa zinazowaka). Manispaa ya Moshi ina mkakati wa kukarabati taa hizo kwa awamu na jumla ya Sh. 155,801,000 zinahitajika kuweka upya taa 330. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Halmashauri imetenga Sh. 25,000,000 kwa ajili ya kuongeza taa za barabarani.

- Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imenunua gari maalum *(Bucket Wagon)* kwa jumla ya Sh. 97,000,000 kutoka kwenye Mfuko wa Halmashauri *(own source)* katika bajeti ya mwaka 2006/2007. Gari hili linatumika kwa ajili ya matengenezo ya taa za

barabarani na limepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za ukodishaji wa magari binafsi. Kwa mwaka wa fedha 2007/2008, barabara zifuatazo zimewekewa taa: Barabara za Kawawa/Nyerere hadi eneo la *Shoprite* (Kamata) taa mpya 62 zimeshawekwa na zinafanya kazi; *TAZARA* Uwanja wa Ndege *(Terminal Two)* taa mpya 60 zitawekwa; na Wizara ya Miundombinu kupitia *TANROAD*, imeanza matengenezo ya taa katika barabara kuu.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kuweka na kukarabati taa za barabarani ni la Halmashauri husika. Napenda kutoa wito kwa Halmashauri zote nchini, kutenga fedha za kutosha katika bajeti zake za kila mwaka kwa ajili ya kuweka na kukarabati taa za barabarani kwa awamu.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amejibu kwamba, Halmashauri ndiyo zenye wajibu; na kwa kuwa Miji haipendezeshwi na taa za barabarani usiku tu, kuna taa nyingi sana za *decorations* za kufanya Miji iwe vivutio na alama maalum; je, kwa nini Miji yetu haina taa hizo na lini Halmashauri zitafanya shughuli hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, mimi naona kwamba, tuanze kwanza na hizo taa za barabarani ambazo ni muhimu, tukimaliza awamu hiyo ndipo tuanze taa nyingine za urembo kupendezesha Miji yetu. Niliona ni muhimu kwanza tuondoe hilo tatizo la giza katika Miji yetu, halafu baadaye hali ikituruhusu, tutaipamba Miji yetu kulingana na bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa taa nyingi za barabarani aidha zinagongwa kutokana na magari yanayopita katika barabara hizo na inachukua muda kurudisha taa hizo kwa sababu ya gharama kubwa ya hizo taa; je, Serikali inazishauri vipi Halmashauri ya Wilaya zote nchini, kuweka sheria kali juu ya magari ambayo yanavunja hizi barabara kwa sababu ya uzembe wa madereva?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Sheria za Barabarani zipo ila tatizo ni utekelezaji. Kwa hiyo, nawashauri au tunawaagiza madereva kuwa waangalifu zaidi katika kutekeleza Sheria za Barabarani. Tatizo kubwa siyo Halmashauri ila tatizo ni wale watekelezaji ambao wanavunja sheria na sheria hizo zipo. Mimi naomba watu watilie mkazo sheria hizo ambazo zimewekwa kwa ajili ya usalama barabarani.

Na. 431

**Mradi wa Umeme Mgwashi**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini ya Mwaka 2006/2007, katika kifungu cha Nishati Vijijini, Mradi wa Umeme Mgwashi Jimbo la Bumbuli ulitengewa Sh. 204,000,000:-

(a) Je, ni hatua gani zimefikiwa katika kutekeleza mradi huo?

(b) Je, wakati huu Waziri ana ushauri gani kwa wananchi wapatao mia sita waosubiri umeme uwafikie?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Mji Mdogo wa Mgwashi uko kilometa 30 kutoka Mbelei, ambako njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 11 inapita kuelekea Mponde. Vijiji vilivyo kati ya Mbelei na Mgwashi ni Kwesine, Baga, Waga na Nkongoi. Ili kupeleka umeme Mgwashi, kunahitajika kujenga laini ya kilovoti 11 ya urefu wa kilometa 30, kujenga laini ya kilovoti 0.5 ya urefu wa kilometa 10, kufunga transfoma tano zenye uwezo wa *kVA* 50 kila moja na transfoma moja yenye uwezo wa *kVA* 100. Gharama ya mradi huo ni Sh. 450,000,000.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini ya mwaka 2006/2007, Serikali ilitenga Sh. 204,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Hata hivyo, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Serikali ilitoa Sh. 100,000,000 tu kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo, kutokana upungufu wa fedha katika bajeti ya Serikali na uwezo mdogo wa kifedha wa Shirika la *TANESCO*, uliosababishwa na sababu mbalimbali ikiwemo ya Serikali kugharamikia umeme wa dharura, baada ya nchi yetu kukumbwa na balaa la ukame na hivyo vyanzo vya umeme wa nguvu ya maji kutoweza kuzalisha umeme wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hatua iliyofikiwa katika kutekeleza mradi huo ni kukamilisha upembuzi yakinifu na kufanyika upimaji wa njia ya umeme *(surveying)* kutoka Mbelei hadi Mgwashi.

(b) Mheshimiwa Spika, naomba kuwashauri Wananchi wa Vijiji vya Kwesine, Baga, Waga, Nkongoi na Mgwashi, waendelee kuvuta subira wakati Serikali inafanya jitihada

za kuwapatia huduma hiyo. Serikali inaelewa umuhimu wa umeme katika eneo lao na inafanya kila iwezavyo ili kutekeleza Mradi wa Umeme Mgwashi.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuishukuru sana Wizara kwa utekelezaji wa mradi huo, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kabla ya kuyauliza ningeomba nifanye masahihisho katika yale majina ya Vijiji pale kwenye Waga ni Wanga, halafu kiongezwe Kijiji cha Malomboi na Sagara katika huo mtandao. Napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa sababu ameanzisha utaratibu ambao ni mzuri sana. Majibu haya mimi niliyapata jana mchana, nadhani huu ni utaratibu mzuri, umeniwezesha kuona ni mahali gani ambapo kuna dosari. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mradi huu umeshakubalika na ulikuwa upate Sh. 204,000,000 mwaka 2006/2007, lakini kwa ajili ya dharura iliyotokea ambapo mimi pamoja na Wananchi wa Mgwashi tunaikubali; je, Waziri haoni sasa kwamba ni wakati muafaka katika zile Sh. 10,000,000,000 zilizopo katika Mradi wa Nishati Vijiji katika mwaka 2007/2008 sasa Sh. 350,000,000 zipatikane ili kufidia upungufu huo maana mradi huu ni endelevu?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa Mradi wa Umeme kutoka Mbelei unapitia katika Kijiji cha Kwakitui uliopo katika Kata ya Mamba; je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba itakuwa ni vizuri kwa wananchi hawa ambao hawapo Mgwashi wakapatiwa umeme huo ili kupunguza gharama ambazo baadaye zitatokea?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza tunaomba radhi kwa kukosea majina ya Vijiji ambavyo Mheshimiwa Mbunge alivitaja na tumezingatia marekebisho ya majina sahihi ya Vijiji ambavyo tulivikosea. Lakini pili, nimshukuru kwa kuipongeza Wizara na tunafahamu jinsi gani Mheshimiwa Mbunge, tumekuwa tukifanya naye kazi kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, katika kujibu nianze na kipengele cha kwanza cha swali. Kama ambavyo tumekuwa tukiliarifu Bunge hili Tukufu na wananchi ni kwamba, utekelezaji wa mradi kutegemea Wakala wa Nishati Vijijini, utaanzia na miradi ambayo imeshafanyiwa kazi awali. Kwa hiyo, kwa sababu maeneo ya Mheshimiwa Mbunge tayari yalishafanyiwa upembuzi yakinifu, tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutazingatia na tutaanza pamoja na miradi mingine, lakini pia miradi yake ambayo imeshafanyiwa upembuzi yakinifu na kwa sababu tulishatoa fedha za kuanzia za awali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, kwenye maeneo ambayo kwa mfano kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kati ya Mbelei na Kwakitui pale kwenye Kata ya Mamba, maeneo ambayo hayajafanyiwa upembuzi yakinifu tunamwahidi kwamba, tutaliagiza Shirika letu la *TANESCO* kwenda kufanya upembuzi yakinifu kujiridhisha na gharama zinazohitajika na kuona kama masuala ya kibiashara, kwa sababu huduma ya umeme inatolewa kibiashara kama kuna mahitaji ambayo yanakidhi kwa kutegemea vigezo ambavyo vinatumika katika kusambaza umeme. Lakini narudia tena kusema kwamba, tunamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote, ambao wamekuwa wakitupa ushirikiano na tunawaomba tuzidi kushirikiana.

Na. 432

**Kuharakisha Shughuli za Utoaji Maamuzi ya Kesi**

**MHE. OMAR S. KWAANGW'** aliuliza:-

Katika jitihada za kuendeleza juhudi za kusikiliza kesi na kutoa maamuzi mapema:-

(a) Je, utaratibu wa Jaji/Hakimu aliyepangiwa kusikiliza kesi au kuiendeleza hadi kukamilika *(individual calendar)* umezingatiwa kwa kiasi gani kwa kutoa mifano halisi katika kuondoa matatizo ya ucheleweshaji unaotokana na kesi kuhamishwa toka kwa Jaji /Hakimu mmoja kwenda kwa mwingine?

(b) Je, utaratibu wa usuluhishi nje ya Mahakama *(Alternative Dispute Resolution)*, ulioanzishwa katika Kanda ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha miaka michache iliyopita, umefanikiwa kwa kiasi gani na je, umeendelezwa nchi nzima?

(c) Je, utaratibu wa kuwasomea washtakiwa wa kesi za mauaji hata kama hakuna vikao maalum vilivyopangwa kwa madhumuni hayo, unatekelezwa kwa kiwango gani hadi kesi zao zinaposikilizwa na unasaidia vipi katika kuharakisha usikilizaji wa kesi hizo mapema?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar S. Kwangw', Mbunge wa Babati Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa *Individual Calendar* umezingatiwa kikamilifu na unatekelezwa na Mahakama za ngazi zote kuanzia Mahakama za Mwanzo hadi ya Rufani. Upo Waraka kuhusu utaratibu wa utendaji wa kazi za Kimahakama, unaelekeza Majaji na Mahakimu kusikiliza mashauri yote yanayopangiwa kuanzia mwanzo mpaka mwisho kulingana na kalenda ambayo kila mmoja wao anatakiwa kuandaa. Kwa kuzingatia utaratibu huu, ucheleweshaji wa kesi unaotokana na kesi kuhamishwa toka kwa Jaji au Hakimu mmoja kwenda kwa mwingine haupo tena.

(b) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa *Alternative Dispute Resolution* kwa sasa bado unaendelea kutumika katika Kanda za Dar es Salaam, Mwanza na Arusha. Utaratibu huo umefanikiwa licha ya matatizo ya kutokuwepo kwa Majaji na Mahakimu wa kutosha na ambao wamepatiwa mafunzo kuhusu utaratibu huo. Kadhalika, baadhi ya Mawakili wa kujitegemea nao wamekuwa hawana utaalam wa kutosha katika kutumia utaratibu wa

*Alternative Dispute Resolution*. Zoezi la kuendeleza utaratibu huo katika Mikoa mingine litaendelea kufanyiwa kadri Majaji na Mahakimu wenye utaalam watakavyoongezeka.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuwapatia mafunzo Majaji na Mahakimu ambao hawajapata mafunzo hayo, pamoja na kuwahamasisha wananchi kutumia utaratibu wa *Alternative Dispute Resolution* kutatua migogoro yao.

(c) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa washtakiwa wa kesi za mauaji kusomewa mashtaka hata kabla vikao maalum havijapangiwa unatekelezwa kikamilifu. Utaratibu ni kuwa, washtakiwa wa kesi za mauaji, husomewa mashtaka kwenye vikao vya kesi za mauaji kila zinapokuwa tayari. Mara baada ya kukamilika kwa zoezi hilo, mashauri yote hupangwa kusikilizwa. Utaratibu huu huharakisha mchakato wa usikilizaji wa kesi za mauaji kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, uteuzi wa hivi karibuni wa Majaji ishirini na moja wa Mahakama Kuu, utasaidia sana kupunguza tatizo la ucheleweshaji wa usikilizaji wa kesi za namna hiyo.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa upo msemo kwamba, haki inayocheleweshwa ni sawa na haki inayonyimwa; na kwa kuwa Mwanasheria Mkuu amesema kwamba utaratibu huu wa *Alternative Dispute Resolution* ni mzuri zaidi na unasaidia sana na unapunguza ucheleweshaji wa kesi; je, sasa Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha utaratibu huu mzuri wa *Alternative Dispute Resolution* ili kuhakikisha kwamba kesi nyingi zinazocheleweshwa hasa zilizoko Mahakama Kuu na hasa za Ardhi na hasa kule Babati ambazo zinagusa wananchi wengi, Serikali inaweza kufanya mipango gani kuhakikisha kwamba utaratibu wa *Alternative Dispute Resolution* kwa kweli unaimarika ili kupunguza kesi hizi?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu swali la awali, mpango huu wa *Alternative Dispute Resolution* utaendelezwa kufuatana na mafunzo ambayo hutolewa kwa Waheshimiwa Majaji na Mahakimu waliobaki. Hivi sasa unatekelezwa katika Mikoa ya Kanda za Dar es Salaam, Mwanza na Arusha tu. Kwa hiyo, mara utaalam huo utakaposogezwa karibu na hawa Waheshimiwa Majaji na Mahakimu, ndipo mpango huo utaendelezwa nchi nzima.

Kwa lile shauri la Babati ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', napenda kumhakikishia kwamba, litakuja kwa ajili ya *trial conference* tarehe 23 Agosti, 2007, mbele ya Mheshimiwa Lugazia wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Kama wahusika kwenye kesi hiyo hawatapatana, basi ndipo kesi hiyo itapangwa kusikilizwa. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira kwani wahenga husema subira yavuta kheri.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kesi za mauaji ni nyingi na Majaji ni wachache. Je, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, atakubaliana na maoni yangu kwamba wakati umefika sasa Hakimu Mkazi Mkuu apewe *extended jurisdiction* ili aweze kusikiliza kesi za mauaji?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, hata hivi sasa ninavyozungumza, Mahakimu Wakazi Waandamizi huwa wanapewa *extended jurisdiction* ya kusikiliza kesi za mauaji. Kwa hiyo, jambo hilo linaendelea hivi sasa.

Na. 433

**Hitaji la Gari Idara ya Ukaguzi**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kitengo cha Ukaguzi wa Elimu katika Shule za Msingi ni muhimu sana ili kuhakikisha kuwa elimu inapewa kipaumbele katika Wilaya ya Magu; na kwa kuwa ukaguzi mzuri ni pamoja na kufika katika maeneo ya shule za msingi na za sekondari, pamoja na kupeleka ruzuku za matumizi mapema; na kwa kuwa Idara ya Ukaguzi wa Elimu Wilaya ya Magu ina gari aina ya Suzuki ambalo halihimili kazi zilizopo; je, Serikai itapeleka lini gari ambalo litahimili mizunguko ya Wilaya ya Magu yenye Kata 27?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Wilaya ya Magu ina gari aina ya Suzuki, ambalo haliwezi kuhimili kazi zote za ukaguzi wa shule. Wizara yangu imekuwa ikinunua magari kwa ajili ya ukaguzi wa shule kila mwaka na kuyasambaza katika Wilaya. Mwaka wa Fedha 2005/2006, ilinunua magari kumi na nane na mwaka wa fedha 2006/2007, ilinunua magari kumi na sita na mwaka huu 2007/2008, imepangiwa kununua magari kumi na tano. Lengo ni kuhakikisha kuwa, Ofisi za Ukaguzi wa Shule za Wilaya zote nchini zinapata vyombo imara vya usafiri. Hivi sasa kuna Wilaya 28 zenye magari ya zamani, ikiwemo Magu na Wilaya 46 hazina magari kabisa. Wizara yangu itaendelea kuziimarisha Ofisi za Ukaguzi za Wilaya kwa kuzipatia magari mapya kwa awamu, kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana. Napenda kuzishukuru Halmashauri za Wilaya kwa ushirikiano mzuri wanaoutoa katika kufanikisha kazi ya ukaguzi wa shule katika maeneo yao hususan Wilaya ambazo hazina vyombo vya usafiri kwa sasa.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kabisa kwamba Wilaya hii ya Magu ina gari aina ya Suzuki ambalo haliwezi

kumudu Kata zote 27 za Wilaya ya Magu; amelieleza Bunge lako Tukufu kwamba mwaka 2007/2008, wanatarajia kununua magari 15; je, Mheshimiwa Waziri haoni sasa kuna haja ya kufanya upendeleo maalum katika Wilaya hii ya Magu wakatupelekea gari moja tu ili liweze kufika maeneo mengi ya Kata hizo 27?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwamba tunapokea ombi lake, lakini tukumbuke nimesema zipo Wilaya 46 ambazo hazina kabisa hata hilo gari bovu. Kwa hiyo, tutaangalia kadri fedha zitakazopatikana, Mheshimiwa Mbunge tunakuahidi tutakusaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa leo ni siku ambayo tunahitimisha Bunge letu kwa Mkutano huu, naomba kwa niaba ya Waziri wangu, nitoe shukrani za dhati kwa namna ya kipekee, Waheshimiwa Wabunge ambavyo wanafuatilia maendeleo ya elimu nchini. Tunaomba wapokee pongezi zetu, pamoja na wananchi ambao tunashirikiana nao sana. Asanteni sana.

**SPIKA:** Pamoja na shukrani hizo, Mheshimiwa Naibu Waziri bado Wabunge wanataka kukuhoji.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa suala la msingi lilikuwa ni Kitengo cha Ukaguzi na ni ukweli ulio dhahiri kwamba, Kitengo hiki cha Ukaguzi ni cha msingi sana kwa sababu ndicho kinachopaswa kuangalia mitaala; kama walimu kweli wanafuata mitaala mashuleni na kama wanafunzi wanafika mashuleni; je, Wizara ina mikakati gani ya kuboresha Kitengo hicho ili kiweze kufanya kazi zake sawa sawa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, ningependa tu kuchukua nafasi hii kumjulisha kwamba, tunapokuwa na mpango wowote ule wa MMES au MMEM, ndani yake huwa kuna sehemu inayoshughulikia suala la ukaguzi. Kwa hiyo, kwa kuwa sasa hivi tunaangalia upya andiko la MMES ni pamoja na kuangalia Idara ya Ukaguzi ambayo ni muhimu sana kama ulivyosema Mheshimiwa Mbunge katika kukagua maendeleo ya elimu mashuleni, ikiwa ni pamoja na kuangalia ufundishaji na mitaala. Kwa hiyo, hilo linazingatiwa hasa katika andiko jipya. Nakushukuru sana.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kumpa taarifa kwamba, gari lile aina ya Suzuki lililoko Magu ni bovu na halifanyi kazi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kama inawezekana katika magari 15 angeahidi moja liende Magu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nashukuru kwa

taarifa yake kwamba, gari hilo ni bovu, hatukuwa na taarifa. Naomba nirudie tena kwamba, tutajipanga vizuri na endapo makusanyo yetu yatakuwa mazuri, basi Magu itapewa kipaumbele.

Na. 434

**Ujenzi wa Mradi wa Umwagiliaji - Misozwe**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa, ujenzi wa Mradi wa Umwagiliaji Maji wa Kijiji cha Misozwe Wilaya ya Muheza ulioanza kujengwa zaidi ya mwaka mmoja uliopita bado haujakamilika; na kwa kuwa, inatia wasiwasi kama utakamilika:-

(a) Je, ni sababu gani za msingi zinazosababisha ujenzi wa mradi huo kuchukua muda mrefu kukamilika?

(b) Je, Wanakijiji wa Misozwe wategemee mradi huo kukamilika lini?

(c) Je, Wilaya ya Muheza ina miradi gani mingine ya umwagiliaji katika Mpango wa Umwagiliaji wa Taifa *(National Irrigation Master Plan)?*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a), (b) na (c), napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, ujenzi wa Mradi wa Umwagiliaji Misozwe ulikadiriwa kugharimu shilingi milioni 450. Kazi zilizokusudiwa kutekelezwa zilijumuisha ujenzi wa bwawa dogo lenye ukubwa wa meta za ujazo 236,200 na kuchimba mfereji mkuu na ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya kuboresha kilimo cha umwagiliaji katika eneo la hekta 100. Aidha, bwawa hili litaweza kutumika kwa matumizi ya maji ya nyumbani na ufugaji wa samaki. Katika bajeti ya mwaka 2004/2005, Serikali ilitenga shilingi milioni 56 kwa ajili ya Mradi wa Misozwe. Kazi zilizofanyika zinajumuisha kusafirisha mitambo na baadhi ya vifaa vya ujenzi hadi eneo la mradi, kutoa mchanga na kuchimba msingi wa tuta la bwawa meta za ujazo 3,230, kuchimba na kukusanya udongo kwa ajili ya ujenzi wa tuta la bwawa kiasi cha meta za ujazo 6,5000, ujenzi wa maumbo ya kutoa maji kutoka kwenye bwawa ikiwa ni pamoja na ufungaji wa mabomba ya chuma na ukarabati wa mitambo ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, kama ifuatavyo:-

(a) Sababu za msingi zinazofanya ujenzi wa Mradi wa Umwagiliaji Misozwe kuchukua muda mrefu kukamilika ni zifuatazo: Ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya kuendeleza miradi ya umwagiliaji maji hivyo kulazimika kutekeleza mradi kwa

awamu; mvua nyingi ambazo zimekuwa zikinyesha katika eneo la Misozwe zilisababisha kazi za ujenzi kusimama mara kwa mara na kuharibika kwa maeneo ambayo yamekwisha kufanyiwa kazi kutokana na mafuriko; na uchakavu wa mashine na mitambo inayotumika ambayo iliingizwa nchini mwaka 1985.

(b) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2007/2008, Wizara yangu itakamilisha kazi kuu za ujenzi wa Bwawa la Misozwe na mfereji mkuu wa umwagiliaji. Aidha, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali kupitia Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP)*, inapeleka asilimia 75 ya bajeti ya maendeleo ya kilimo katika Wilaya. Kwa hiyo, kazi za kukamilisha mradi zinazojumuisha ujenzi wa mifereji na miundombinu midogo midogo, zitategemea upatikanaji wa fedha zitakazotengwa na Halmashauri ya Wilaya chini ya Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs).* Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza haikuingiza Mradi wa Misozwe katika Mpango wake wa Maendeleo ya Kilimo wa 2007/2008, Wizara yangu itashirikiana na Halmashauri hiyo kuhakikisha kwamba, kazi zilizobaki zinaingizwa katika Mpango wa *DADP* wa 2008/2009.

(c) Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Muheza inayo miradi mingine miwili ya Umwagiliaji ambayo imeorodheshwa katika Mpango Kabambe wa Umwagiliaji wa Taifa *(National Irrigation Master Plan – NIMP),* Miradi hiyo ni: Potwe (hekta 40) na Kitivo/Maduma (hekta 300). Hata hivyo, Wizara yangu inashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, kubaini miradi mingine ambayo inaweza kuwa ilisahaulika ili iingizwe katika Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu aliyoyatoa, lakini naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa tatizo moja kubwa lililosababisha kucheleweshwa kwa mradi huo ni uchakavu wa vifaa mitambo ambayo kwa kweli ipo pale kijijini hadi sasa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba vifaa vipya vinapatikana hasa ukizingatia kwamba Kitengo hiki kinafanya kazi kwa ufasaha sana lakini kinaelemewa kutokana na uchakavu wa mitambo hiyo?

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa mradi wenyewe unaelekeza katika utekelezaji wa ujenzi wa bwawa, mifereji pamoja na miundombinu. Lakini mahitaji ya wananchi ni pamoja na ujenzi wa skimu ambao wanakijiji wameiomba Wizara iwasaidie katika kuandika mwandiko wa kuwezesha wao kupata fedha. Je, suala hilo litakuwa limefikia wapi hadi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, kuhusu vifaa chakavu kama nilivyosema katika swali la msingi, vifaa hivi viliingizwa nchini mwaka 1985 kwa ajili ya ujenzi wa Miradi ya Kitigo, Lushoto na Mwamapuli kule Tabora na ndivyo vinaendelea kutumika.

Sasa kuhusu kununua vifaa vipya labda nimkumbushe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, hivi sasa Serikali imejitoa kwenye kazi hizi za kununua vifaa na kujenga

barabara na miradi. Utaratibu unaotumika ni wa kutumia sekta binafsi ili iweze kujenga miradi hiyo. Kwa hiyo, Serikali kwa kweli haina mpango wowote wa kuanza kununua *bulldozers* na *excavators* kwa ajili ya kujenga miradi ya umwagiliaji. Tunachofanya hivi sasa ni kuhakikisha kwamba, sekta binafsi inakua, inapata uwezo wa kujenga miradi kama hiyo. Hata hivyo, tunaendelea kutumia vifaa vilivyopo kwa kununua *spare* kwa sababu baadhi ya miradi si mikubwa, haiwavutii sekta binafsi kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuandika *write-up*, hii ni kazi ambayo inaendelea. Kama uandishi wa Mradi wa Skimu wa Misozwe ulikuwa bado haujakamilika, basi namuahidi nitafuatilia, hili ni jambo rahisi kabisa na tutakamilisha.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri. Pili, kwa kuwa Wilaya ya Namtumbo nayo ina miradi ya umwagiliaji iliyo katika Mpango wa Taifa *(Naitonal Irrigation Master Plan)*; je, Mradi wa Liuni Namtumbo, Serikali imeweka mkakati gani wa kumalizia miundombinu yake mwaka huu wa fedha ili wakulima kutoka katika Kata za Namtumbo, Luegu, Mkongo, Gulioni na Mchomolo wanaotegemea mradi huo waweze kulima kama ilivyokusudiwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Liuni ni mradi ambao unaendelea. Kwa sababu mradi huu unaendelea, basi sisi kwa kawaida tunatoa kipaumbele kwa kukamilisha viporo. Nataka nimuahidi na nimhakikishie kwamba, Mradi wa Liuni utakamilishwa.

Na. 435

**Kuanzishwa Kwa Ranchi ya Serikali - Ludewa**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

Kuwa kuwa, maeneo mengi ya Ludewa hasa yanayozunguka machimbo ya Liganga yanafaa sana kwa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na wa nyama; na kwa kuwa, soko la nyama na maziwa litaongezeka sana kutokana na machimbo ya Liganga na Mchuchuma; je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha ranchi ya Serikali maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wilaya ya Ludewa inazo fursa nyingi zinazoweza kutumika katika kuendeleza ufugaji. Fursa hizo ni pamoja na hali nzuri ya hewa na eneo la malisho linalofaa kwa ufugaji ambapo takriban hekta 107,918. Wilaya ina ng'ombe 30,754, mbuzi 20,684, kondoo 5,763, nguruwe 10,708 na kuku 124,802. Kutokana na idadi hii ndogo ya mifugo hususan ng'ombe ni wazi kuwa upo

uwezekano mkubwa wa kupanua shughuli za ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na nyama na mifugo mingine Wilayani Ludewa. Aidha, Wilaya ina miundombinu mbalimbali ya mifugo, ikiwa ni pamoja na majosho 16, machinjio mawili madogo, pamoja na vituo viwili vya afya ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, vilevile nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuanza kuvunwa kwa rasilimali za madini zilizomo Wilayani humo katika maeneo ya machimbo ya Liganga na Mchuchuma, kutachochea mahitaji ya nyama, maziwa na mazao mengine ya mifugo kutokana na pato la wananchi wa maeneo hayo kukua sambamba na ongezeko la walaji. Hivyo ni dhahiri kwamba, ipo haja ya kuanzisha vyanzo vya uhakika vya upatikanaji wa mazao hayo, ikiwa ni pamoja na kuanzisha ranchi na mashamba ya mifugo pamoja na maduka ya mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, kama sote tunavyofahamu, jukumu la Serikali kwa sasa ni kuandaa sera, kusimamia sheria na kuratibu maendeleo ya sekta. Sekta binafsi inatarajiwa kuendesha shughuli za uzalishaji, usindikaji, pamoja na shughuli nyingine za mifugo ukiwemo ufugaji wa ranchi na mashamba ya mifugo na utoaji wa huduma nyingine.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli huu na kutokana na fursa nilizoainisha, napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, kubaini eneo halisi litakaloweza kutumika kuanzisha ufugaji wa ranchi na kuwasiliana au kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(Tanzania Investment Centre)* ili kupata wawekezaji makini na wenye nia ya dhati ya kuanzisha ufugaji wa ranchi katika Wilaya hiyo. Sambamba na hili, namshauri Mheshimiwa Mbunge aendelee kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya, kuwashawishi na kuwahimiza wananchi Wilayani humo, kuibua miradi mbalimbali ya ufugaji ukiwemo ufugaji wa ranchi kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(District Agricultural Development Plans – DADPs).* Wizara yangu kwa upande wake itakuwa tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, kutoa utaalam katika shughuli za ufugaji ukiwemo ufugaji huo wa ranchi.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo ndiyo yenye wataalamu na utaalamu wa kuruhusu kuendesha ranchi; je, Waziri anayehusika au Naibu wake, wanaweza kuitembelea Wilaya ya Ludewa haraka iwezekanavyo ili kukutana na uongozi wa Ludewa kusudi watusaidie kuhamasisha na kuangalia maeneo haya ninayoyazungumzia kwamba yanafaa na watushauri kadri inavyowezekana?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, Wizara inakubali na mimi mwenyewe binafsi nitakuwa tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge ili kuitembelea Wilaya ya Ludewa, kuangalia fursa hizo anazozizungumza, pamoja na fursa nyingine katika kuendeleza Sekta za Mifugo Wilayani Ludewa.

Na. 436

**Matatizo Yaliyosababishwa na Wakimbizi Nchini**

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika wema wa kuhifadhi Wakimbizi wengi, Tanzania imekumbwa na uharibifu mkubwa wa mazingira na kuhatarisha usalama wa raia wake; je, vyombo kama *Commonwealth, African Union, EU, African Development Bank* na Benki ya Dunia, vimeisaidiaje Tanzania katika kukabiliana na kutatua tatizo hilo?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (K.N.Y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mbunge wa Morogoro Kusini, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, kutokana na wema wa kuhifadhi Wakimbizi, Tanzania imekumbwa na uharibifu mkubwa wa mazingira na matatizo mengine ya kiusalama kwa raia wetu. Lakini inafaa pia ieleweke kuwa, tuliwapokea Wakimbizi hao kama wajibu wetu wa ujirani mwema na pia kwa kuzingatia wajibu wetu katika Mikataba ya Kimataifa inayohusu Wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mbunge wa Morogoro Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla katika kuwahudumia Wakimbizi, tumepewa ushirikiano mzuri wa Jumuiya ya Kimataifa kupitia Shirika la *UNHCR*, zikiwemo nchi na Mashirika mbalimbali. Idadi ya Wakimbizi wa Rwanda, Burundi na *DRC*, imewahi kufikia zaidi ya 1,380,000 na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira. Serikali yetu kwa kushirikiana na Jumuiya na Taasisi za Kimataifa, ilibuni na kuanzisha miradi mbalimbali, ambayo inalenga kupunguza au kuzuia uharibifu wa mazingira, pamoja na miradi ya kuimarisha usalama katika maeneo yaliyoathirika na Wakimbizi. Baadhi ya miradi iliyobuniwa ilikuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ambayo ilianzishwa mwaka 1996, chini ya Mradi unaoitwa *Special Projects in Refugee Affected Areas (SPRAA).*

Mheshimiwa Spika, ipo pia miradi inayofadhiliwa na kutekelezwa na nchi moja moja au Mashirika na Taasisi za Kimataifa kupitia *UNHCR* au Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Mashirika au Taasisi kama vile *ECHO*, *CARE*, *IRC*, *NPA*, *TCRS* ni miongoni mwa wafadhili wa baadhi ya miradi inayohusiana na mazingira. Kwa sasa upo mradi mkubwa unaofadhiliwa na Serikali ya Denmark, kupitia Shirika lake la Maendeleo *DANIDA.* Mradi wa sasa 2007 – 2009 ni wa *Danish Kroner (DKK)* milioni sitini sawa na shilingi 10bn ya fedha za Kitanzania. Hii ni awamu ya pili baada ya kukamilika ule wa awamu ya kwanza (2003 -2006), uliokuwa na thamani ya milioni sitini *DKK*, sawa na shilingi 8.9bn. Mradi huu unatekelezwa katika maeneo yaliyoathirika na uwepo na

Wakimbizi katika Mikoa ya Kagera na Kigoma. Aidha, juhudi bado zinafanyika kuona uwezekano wa kupata miradi mikubwa zaidi ya aina hii.

Kuhusu Usalama wa Raia, Umoja wa Ulaya *(EU)*, umekuwa unagharamia gharama za askari wanaopelekwa kuimarisha ulinzi na usalama katika Makambi ya Wakimbizi na maeneo jirani. *EU* kupitia *UNHCR*, imekuwa ikitoa msaada huu kupitia Mikataba Maalum kati ya Serikali na *UNHCR (Security Package).* Mwaka wa fedha 2006/2007, ilitoa kiasi cha shilingi 658,256,300.00 kwa ajili hiyo.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Tanzania sasa tunajaribu kuwashawishi Wakimbizi warejee kwao na wengi wanarejea kwao kwa ushawishi huo. Je, sehemu ile ambapo Wakimbizi wameondoka; nani anasimamia urejeshaji wa mazingira sehemu ambazo Wakimbizi wameharibu ni sisi ama tunasaidiwa?

**SPIKA:** Ningependa kufafanua kwamba, anayejibu maswali haya hivi sasa ni Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Capt. John Z. Chilligati, hasa kwa wale wageni, maana yake hili swali limeelekezwa Wizara ya Mambo ya Ndani, lakini utaratibu wa Serikali ni kwamba, Waziri yeyote anaweza kujibu kwa niaba ya mwenzie.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa ufafanuzi huo. Kwa maelewano tuliyonayo kati ya Serikali na Shirika linalowahudumia Wakimbizi Duniani ni kwamba, maeneo yale ambayo Wakimbizi wanaondoka kwanza, eneo lote lile na miundombinu yote iliyopo katika eneo lile, kuna miundombinu, kuna maji katika maeneo yale, shule katika maeneo yale, hospitali zinakabidhiwa Halmashauri za Wilaya kwenye maeneo yanayohusika.

Miradi hii niliyoitaja kama huu wa Denmark bilioni kumi, unaelekezwa katika maeneo hayo na Halmashauri zinazohusika ndizo zinazopewa fedha hizi ili kuweza kurekebisha mazingira yaliyoharibiwa na Wakimbizi.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa hiyo *privilege*. Ni kweli kwamba uwepo wa Wakimbizi katika nchi yetu umesababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na kuhatarisha usalama. Lakini kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba tunatimiza wajibu wetu na pia kuzingatia mikataba ya Kimataifa.

Sasa kwa kuwa Wakimbizi wengine wanaopita hapa si lazima waje Tanzania, wamelenga kwenda nchi kama Afrika Kusini hasa wanaotoka Ethiopia na Somalia; je, Serikali yetu ina mkakati gani wa kuwahakikisha *save pass* ili waweze kupita na kuelekea kule wanakokwenda badala ya kuwakamata na kuwarudisha kule wanakotoka na kusababisha wawe wanajifungia kwenye malori?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kwa Sheria za Kimataifa kuhusu Wakimbizi, mkimbizi ni yule ambaye anatoka katika nchi yake anaingia kwenye nchi ya jirani, huyo ndiyo mkimbizi. Mtu anayetoka katika nchi yake anavuka nchi ya kwanza, ya pili na ya tatu, anakwenda Afrika ya Kusini, huyo sio mkimbizi, huyo ni mhamiaji haramu anakamatwa na kurudishwa alikotoka.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha ameeleza kwamba, tunafaidika vilevile na miundombinu ambayo inapatikana hawa Wakimbizi wanapoondoka na ameeleza hususan miundombinu ambayo ni huduma za jamii kama maji.

Kwenye jimbo langu ipo Kambi ya Wakimbizi ya Lugufu na moja ya miundombinu iliyopo pale ni hospitali nzuri tu na Kambi ile kwa mujibu wa taratibu zilivyo sasa ni kwamba, wakiondoka inafungwa. Lakini kwa utaratibu wa *UNHCR*, Serikali yetu haikabidhiwi vifaa vya hospitali. Wizara inaonaje ili kusaidia wananchi wa eneo lile ambao wameathirika sana kuhifadhi Wakimbizi, vifaa vile vya hospitali viweze kubaki pale na kuwasaidia Watanzania katika eneo lile?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, makubaliano tuliyonayo kati ya Serikali na *UNHCR* ni kwamba, tunapofunga Kambi fulani miundombinu iliyopo inakabidhiwa kwa Serikali ya Tanzania na sisi tunaikabidhi kwenye Halmashauri ya Wilaya inayohusika.

Ni kweli kule kwake Mheshimiwa Mbunge, kuna Kambi mbili; Lugufu A na Lugufu B na hivi karibuni moja ya Kambi hizo ilifungwa kwa sababu Wakimbizi hao ni wa *DRC*, ndio wako katika maeneo hayo, wanazidi kupungua na wakishaondoka hiyo Kambi ikifungwa, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, miundombinu yote iliyoko pale, pamoja na hospitali ile na vifaa vilivyomo vyote vitabaki katika eneo hilo, vihudumie wananchi wa eneo hilo.

Na. 437

**Uhaba wa Watumishi Hospitalini Mikoa ya Pembezoni**

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mikoa ya Pembezoni ina upungufu mkubwa wa watumishi wa kada za *Clinical Officer* na *Nurse Midwives.* Je, Serikali haioni kuwa, ni muhimu kuendeleza utamaduni wa kuwafundisha wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Nne katika Vyuo vya *Pre-Service* kuliko kuwaacha wakizagaa mitaani?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ina upungufu mkubwa wa watumishi wa kada zote za afya wakiwemo Maafisa Tabibu na Wauguzi. Watumishi waliopo katika vituo vyetu vya kutolea huduma za afya ni asilimia 32 tu ya ikama inayohitajika. Upungufu huu ni mkubwa zaidi katika maeneo ya vijijini kuliko mijini.

Mheshimiwa Spika, kwa kulitambua hilo, Serikali kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ilitoa kibali cha kulegeza masharti ya ajira kwa watumishi wa kada za afya ili baada ya kuhitimu mafunzo yao, Wizara yangu iweze kuwapanga watumishi hao moja kwa moja kwenye Mikoa na Halmashauri za Wilaya, kwa kuzingatia nafasi zilizoidhinishiwa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina vyuo vinane vinavyotoa mafunzo ya utabibu *(Clinical Officers)* na vyuo kumi na vitatu vinavyotoa mafunzo ya wauguzi. Wenye sifa za kujiunga na vyuo hivi ni wahitimu wa Kidato cha Nne na cha Sita, ambao walifaulu walau masomo ya sayansi (Fizikia, Bailojia na Kemia) katika mitihani yao ya kuhitimu.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), uliozinduliwa hivi karibuni, suala la upungufu wa watumishi limepewa uzito unastahili. Wizara kwa kushirikiana na wadau wangine inaendelea na mikakati ya kuongeza udahili wa wanafunzi kwa asilimia 40 katika vyuo vya afya vikiwemo vyuo vya utabibu na uuguzi. Mikakati hii inakwenda sanjari na kupanua vyuo vilivyopo kwa kuongeza madarasa, wakufunzi, vifaa vya kufundisha na kujifunzia, maabara na mabweni. Aidha, mpango wa kuanzia kudahili wanafunzi watakaokuwa wanakaa nje ya vyuo (*off-campus)* unaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, huku nikimpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa moyo wake wa kuwajali vijana wetu na kuitakia mema sekta ya afya, aidha, napenda kumshauri yeye pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine kuwashawishi vjana wenye sifa wawasilishe maombi ya kujiunga na vyuo vya afya.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imeamua kuanza mpango wa kutaka kuwadahili wanafunzi ambao watakaokuwa wanakaa nje ya vyuo; je, mpango huo utaanza lini?

La pili, kwa kuwa kuna wanafunzi wengine ambao watakuwa hawana uwezo kabisa wa kuweza kukaa nje ya vyuo; je, Serikali inasemaje?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba mpango wa kuanza kudahili wanafunzi unaandaliwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge avute subira ili tufanye mpango kwa sababu lazima kuwe na maandalizi kwa wale ambao wanatakiwa, pamoja na maandalizi ya kuwa na mabweni walimu na kadhalika, namhakikishia kuwa hili litawezekana.

Swali lake la pili ameonyesha hofu kwa wale ambao watakaokaa nje ya vyuo na hawana uwezo. Naomba niseme kwamba wale ambao watakuwa wanakaa nje ya vyuo ambao hawana uwezo wakati tutakapoangalia utaratibu wa kudahili wanafunzi wengi tutaweza kuangalia ni jinsi gani tutaweza kuwasaidia. Lakini nimwambie tu kwamba asije akafikiri kwamba tutakuwa na utaratibu wa kuomba mikopo kwa sababu hili bado hatujaanza kulizungumza katika Wizara yetu. Lakini namhakikishia kwamba tutahakikisha kwamba wanaokaa *off campus* watakuwa na uwezo wa kupata haya mafunzo ili kuongeza idadi ya wahitimu.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa upungufu wa *Nurse Midwives* ni tatizo kubwa nchi nzima, je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaendeleza pamoja na kuwapa vifaa wakunga wa jadi ili wasaidie katika kupunguza matatizo haya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna upungufu mkubwa wa *nurse midwives* katika vituo vyetu vya kutolea huduma na ni kweli tunatambua umuhimu na kazi wanayoifanya wakunga wa jadi.

Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba upo utaratibu ambao katika Wilaya zetu zote na katika Halmashauri Wakunga wa Jadi kwanza wanatambuliwa na vilevile kuna programu maalumu ambayo wanapewa kupita katika hospitali zetu katika Wilaya kuwapa mafunzo ili kuweza kutambua mgonjwa gani wanaweza kumuhudumia na mgonjwa gani wanatakiwa kumfanyia rufaa.

Vilevile katika programu hii wakunga wa jadi hawa huwa wanapewa vifaa vya msingi ambavyo wanatakiwa kuvitumia wakati wanawahudumia wagonjwa hawa vikiwemo vifaa vya kuhakikisha kwamba wanaweza pia kujikinga au kuambukiza wale wanaowahudumia au kuwaambukiza wao wakati wanapotoa huduma hizi.

Na. 438

**Daraja Kati ya Kijiji cha Ngumbaru na Sokoni Lawate**

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Ngumbaru – Siha wamekuwa wakililalamikia daraja linalovuka kwa karibu kwenda sokoni Lawate; na kwa kuwa daraja hilo limekuwa kero kubwa na taabu kwa watoto wa shule hasa wakati wa masika hushindwa kuvuka ili kuhudhuria masomo yao; na kwa kuwa kijiji hicho pamoja na vijiji jirani vya Ngaritati; Donyomorua na Makiwari vyenye wakulima na wafugaji wengi vinataabika sana kutona

na ubovu wa daraja hilo; Je, ni kwa nini Serikali Kuu isiingilie kati kusaidia ujenzi wa daraja hilo hasa ikizingatiwa kuwa uwezo wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai ni mdogo?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mbunge wa Siha, kama ifuatavyo:-

Kama alivyoeleza kwenye swali lake, daraja hili lipo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Hai. Daraja hilo linaunganisha vijiji vya Ngumbaru, Ngaritati, Donyomorua na Makiwari. Kwa sababu ufinyu wa Bajeti, Wizara yangu haiwezi kusaidia ujenzi wa daraja hilo kwa sasa.

Kwa hiyo, ninamshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Halmashauri husika ili waliweke daraja hilo kwenye mipango yao ili lijengwe kwa kutumia vyanzo vyake vingine vya fedha. Wizara yangu kupita Wakala wa Barabara Mkoa wa Kilimanjaro ipo tayari kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya ujenzi wa daraja hilo kama ushauri huo utahitajika.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa hata mimi mwenyewe sikutegemea kwamba Wizara ya Miundombinu ndiyo itakayonijibu swali hili; na kwa kuwa Serikali ni moja, nilitegemea TAMISEMI ndiyo ambayo ingejibu swali hili; je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kusaidia daraja hili ambalo nimeeleza hapa kwamba ni daraja linalohudumia jamii kubwa na pana sana.

La pili je, pale inapothibitika kwamba Halmashauri haina uwezo na hasa ukizingatia ukweli kwamba sasa Halmashauri ya Wilaya ya Siha ni Wilaya changa hivi utaratibu ukoje tunaendelea kuwaambia wale wanaohusika waendelee kujikuna wao wenyewe au Serikali ina utaratibu wa kuingilia kati na kusaida maendeleo ya Halmashauri husika?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali ni moja na ndiyo maana swali hili tunalijibu sisi. Lakini niseme moja tu umuhimu wa kusaidia upo kwa sababu pale wananchi wameonyesha dhamira yao ya kujiletea maendeleo na niseme tu kwamba katika historia ya daraja hili tangu daraja la muda lichukuliwe na maji wakati wa mvua za *elnino*, wananchi wa Wilaya ya Siha wamejitahidi sana kupitia Mbunge wao kukusanya nguvu zao wenyewe.

Walikusanya shilingi milioni 25 na daraja hili la kudumu linahitaji shilingi milioni 150, tunaamini wakihamasishwa kidogo Serikali na yenyewe kwa upande wake itaweza kufanya kile ambacho inaamini inaweza ikasadia. Tunatambua kabisa kwamba Halmashauri ya Siha ni mpya lakini wajibu wa kuleta maendeleo kwa wananchi na hasa kwa hamasa yao inabaki pale pale, Serikali itachangia pale ambapo inaona kuna jitihada hizo.

Na. 439

**Barabara ya Singida - Karatu**

**MHE. MGANA I. MSINDAI (K.n.y. MHE. LAZARO S. NYALANDU)** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Singida – Mtinko –Lambi – Karatu ni barabara inayounganisha Mikoa ya Singida na Manyara na Arusha; na kwa kuwa barabara hiyo inatoa huduma kupitia Hospitali ya Kitinko, Hospitali ya Lambi, Hospitali Kuu ya Rufaa ya Hydom na hivyo inasaidia kuokoa maisha ya watu, kuharakisha maendeleo ikiwa ni pamoja na kuendeleza utalii kati ya Mbuga za Wanyama za Sengereti, Manyara na Ngorongoro, uwindaji wa utalii wa kijamii (*Cultural tourism*) katika Mkoa wa Singida: (a) Je, Serikalio itakubaliana nami kwamba barabara hiyo inastahili kujengwa kwa kiwango cha lami? (b) Je, ni lini upembuzi yakinifu na ujenzi wa barabara hiyo utaanza?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Singida – Karatu ni barabara ya mkoa yenye jumla ya urefu wa kilomita 246.5, ambayo inaunganisha Mikoa ya Singida, Manyara na Arusha. Sehemu kubwa ya barabara hii ni ya changarawe na inahudumiwa na Mikoa niliyoitaja kama ifuatavyo:- Wakala wa Barabara Mkoa wa Singida inahudumia sehemu ya Singida, Ilongero, Nkungi hadi Kidarafu yenye urefu wa kilometa 83. Sehemu ya Kidarafu hadi Kilimapunda yenye urefu wa kilometa 113.5 inahudumiwa na Wakala wa Barabara Mkoa wa Manyara na sehemu ya Kilimapunda – Karatu yenye urefu wa kilomita 50 inahudumiwa na Wakala wa Barabara Mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaelewa umuhimu wa barabara hii, hivyo imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya matengenezo kadri bajeti inavyoruhusu. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Serikali kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* katika Mkoa husika ilitumia jumla ya shilingi milioni 954.344 kuifanyia matengenezo barabara hii ili kuiwezesha kupitika katika kipindi chote cha mwaka. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 1,600,693 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hii. Matengenezo haya yatahusisha matengenezo ya vipindi maalumu, madaraja, sehemu korofi na matengenezo ya kawaida ili barabara hii iweze kupitika kwa kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti kwa hivi sasa, Serikali haina mpango wa kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, Serikali itaendelea

kutenga fedha za matengenezo kila mwaka ili kuhakikisha kuwa barabara hii inapitika vizuri majira yote ya mwaka.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwanza, napenda kuipongeza Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara hii kwa kiwango cha changarawe.

Kwa kuwa eneo kati ya Ilongero kupitia Kungi yaani Iyambi, Idarafa mpaka Hydom huwa linasumbua sana wakati wa masika; je, Serikali itakuwa tayari kwa hizi fedha za 2007/2008 itengeneze kipande hicho ili watu waendelee kupita wakati wote?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, tunapokea pongezi zake alizozitoa lakini pili kuhusiana na kipande hicho alichokitaja cha kutoka Ilongero Iyambi hadi Hydom tunakifahamu ni sehemu korofi kidogo na ndiyo maana ukiangalia bajeti yetu ya mwaka huu wa fedha eneo hili ambalo amelitaja Mheshimiwa Mbunge ni sehemu ya barabara hiyo ambayo itafanyiwa matengenezo katika mwaka huu wa fedha.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umefika. Ninayo matangazo machache kuhusu hapa wageni. Kwanza, ni wageni wa Mheshimiwa Christina G. Ishengoma, Mbunge ambaye ameapishwa leo asubuhi hii, wa kwanza ni mume wake Prof. R.C Ishengoma ambaye pia ndiye Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro. Naona familia hii imebarikiwa sana maana yake, mume ni Profesa, Meya. Mke ni *Doctor*, Mbunge na Mkuu wa Mkoa wa Pwani. (*Makofi*)

Pamoja na waliomsindikiza ni Bi Getrude Mpaka ambaye ni Afisa Tawala wa Mkoa wa Pwani, yule pale! Paskazia George mwanae Mbunge, pamoja na watoto wengine ambao ni Anaeli Irene na Fredrick. Wale pale, karibuni sana, na ndugu na jamaa ambao hawakutajwa nadhani wale wengine wote waliosalia wasimame, ahsante sana! Karibu sana na ahsante kwa kumsindikiza Mbunge mpya.

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Felista Bura anaitwa Ndugu Vanesa Mgeta ni Afisa Habari wa Chuo Kikuu Huria yule pale! Halafu Mheshimiwa Sigfrid Ng'itu, ana mgeni wake ambaye ni mwanae Ndugu Gana Ng'itu, ni mwanafunzi wa Sheria Chuo Kikuu cha Tumaini. Mheshimiwa Musa Azzan Zungu ana mgeni wake anaitwa Haji Manara yule pale karibu sana. Mheshimiwa Telele ana wageni kutoka Ngorongoro na Morogoro ambao hakuwataja majina. Sasa wageni wa Mheshimiwa Telele wale pale! Hawa kweli wanatoka Ngorongoro, karibuni sana! Kuna ujumbe wa wanamtandao wa Wachimbaji Madini Afrika, Tawi la Tanzania wakiongozwa na Mwenyekiti wao Bi. Helen Kimoro. Naomba wasimame, wale pale! Karibuni sana. Huu ndiyo ujasiriamali ambao Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete anauhimiza na inapendeza kweli kuona akina mama mnajibidisha katika masuala ya madini. Tunawatakia mafanikio.

Wapo wanafunzi 15 kutoka Chuo Kikuu cha Tumaini wakifuatana na mlezi wao Ndugu Asheseta Lema, pamoja na kiongozi wao ambaye ni Rais wa Serikali ya Wanafunzi, Ndugu Sweatbart Mkoba. Naomba wasimame tafadhali. Tunawatakia

maandalizi mema na mafanikio katika masomo. Wapo pia wanafunzi 40 na walimu wawili kutoka shule ya Hijra Seminari, baadhi yao kundi moja lilitangulia jana na leo nadhani tuna kundi jingine. Walimu na vijana wa Hijra Seminari msimame tafadhali. Karibuni tunawatakia mema katika masomo yenu, nchi inawahitaji sana.

Waheshimiwa Wabunge, Kampuni ya Tanzania *School Equipments* imekuja na vifaa vya shule vinapatikana katika eneo letu la tafrija pale kwenye jengo la utawala. Waheshimiwa Wabunge wote mmewekewa kila mtu shehena yake, hakuna masharti yoyote kuvipata vinatolewa bure. Kwa hiyo, baada ya kuahirishwa Bunge mpite pale kwenye eneo la tafrija kujikusanyia vifaa.

Napenda kutambua vazi rasmi na linalopendeza sana la Mheshimiwa Mbunge wa Kyela Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe. Namwomba asimame ili muweze kumwona. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Kawawa ni kawaida yake siku za Ijumaa lakini Mheshimiwa Harrison Mwakyembe sijawahi kumwona akiwa hivyo. Pengine Mheshimiwa Kawawa utamsaidia leo Mheshimiwa wakati wa swala ya Ijumaa kumsindikiza katika Msikiti Mkuu pale, ahsante sana. Katibu kwa utaratibu unaofuata.

**UCHAGUZI WA WAJUMBE KWENYE BODI ZA VYUO VIKUU MBALIMBALI VYA ELIMU YA JUU NCHINI**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tuna hatua fupi leo ya kufanya uchaguzi wa wajumbe watakaotuwikilisha katika Bodi za Vyuo Vikuu mbalimbali vya Nchi yetu kama ambavyo imeorodheshwa pale. Chule Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Chuo Kikuu Kishiriki cha Muhimbili, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Ardhi na Chuo Kikuu cha Mzumbe. Utaratibu nadhani tutakwenda haraka sana kwa sababu kampeni zilikwishafanyika na takriban kila nafasi ina wale tu wanaohusika kuchaguliwa.

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge kama nilivyotangaza siku ya Ijumaa ya tarehe 10/8/2007 na Alhamis tarehe 16/8/2007, kuwa leo tarehe 17/8/2007 baada ya kipindi cha maswali kama ilivyo kwenye *order paper* kutakuwa na uchaguzi wa Waheshimiwa Wabunge watakaoliwakilisha Bunge hili katika Mabaraza ya Vyuo Vikuu vifuatavyo:-Chuo Kikuu cha Sayansi ya Afya Muhimbili, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Ardhi.

Muda wa mwisho wa kurudisha fomu za kuomba uteuzi ilikuwa ni Jumatano tarehe 15/8/07 saa saba mchana na baadaye muda uliongezwa hadi tarehe 16/8/ 2007 saa kumi jioni. Muda huo uliopofika Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wamejitokeza kuchukua fomu na kuzirejesha ni wanane kwa mpangilio unaofuata: Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili ni nafasi mbili na waliochukua fomu ni wawili: Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba na Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya. Chuo Kikuu cha Mzumbe ni nafasi moja, hapa waliochukua fomu ni wawili nao ni wafuatao: Mheshimiwa Magdalena K. Sakaya na Mheshimiwa Martha Umbulla. Chuo Kikuu cha Sokoine cha

Kilimo nafasi moja, aliyechukua fomu ni mmoja naye ni Dr. Mzeru Nibuka. Chuo Kikuu cha Dodoma ni nafasi moja na aliyechukua ni Mheshimiwa Job Ndugai. Chuo Kikuu cha Ardhi nafasi ni mbili, waliochukua fomu ni wawili nao ni Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Aloyce Kimaro.

Mheshimiwa Spika, uchaguzi huu unaendeshwa kwa kufata masharti ya Kanuni ya (9)A ya nyongeza ya pili ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004 ambazo zinafafanua taratibu za uchaguzi wa Wabunge wanaokwenda katika vyombo ambavyo kwa mujibu wa Sheria vilivyounda vyombo hivyo vinatakiwa viwe na uwakilishi wa Bunge.

Aidha, kifungu cha 2.2 (b)(iii) ya nyongeza hiyo kinafafanua kuwa endapo atajitokeza mgombea mmoja wa nafasi inayohusika, Wabunge watapiga kura za NDIYO au HAPANA. Kwa mantiki hiyo kwa upande wa Vyuo vya Muhimbili, Sokoine, Dodoma, na Ardhi wagombea watapigiwa kura za NDIYO au HAPANA. Isipokuwa kwa Chuo Kikuu cha Mzumbe ambapo wagombea waliojitokeza ni wawili na anatakiwa mmoja.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 2.2 (a) cha nyongeza ya pili ya Kanuni za Bunge, kila mgombea atatakiwa afike mbele ya Waheshimiwa Wabunge yaani wapiga kura kujieleza kwa dakika zisizozidi tatu na kujibu maswali yao na kama yatakuwepo baada ya kujieleza karatasi za kupiga kura zitatolewa kwa kila mpiga kura.

Mheshimiwa Spika, hapa ni mwisho wa maelezo ya Katibu wa Bunge kama msimamizi wa Uchaguzi huu, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka tulikwishaweka utaratibu pale ambapo hakuna ushindani hatulazimiki kupiga kura tena ya NDIYO au HAPANA. Kwa hiyo, nitamwomba Katibu atupe karatasi tu pale ambapo kuna ushindani halafu tugawiwe karatasi za kura na pale ambapo hakuna atawatamka, tutawahoji na ndiyo watakuwa wamepita. Katibu!

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, naomba kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba baada ya mazungumzo na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, amekubali kujitoa na kumwachia Mheshimiwa Umbullah. Ameniagiza.

**KATIBU WA BUNGE:** Kutokana na maelezo hayo na kama pendekezo hilo linakubalika maana yake ni kwamba walioomba nafasi hizo wanalingana na nafasi zilizopo na kwa pendekezo ambalo limetolewa la kwamba huko nyuma tumewahi kusema kwamba waliogombea kama wanalingana na nafasi zile basi wapite bila kupingwa.

**MHE. ANNE. M. ABDALLAH:** Mwongozo wa Spika! Naomba tu Mwongozo wako. Katika hali hiyo iliyojitokeza tutakuwa na uhakika gani kwamba Mheshimiwa Sakaya amejiondoa? Kwa sababu mtu anapojiondoa rasmi kwenye uchaguzi anapaswa kutoa taarifa ya maandishi. Nauliza inawezekana?

**SPIKA:** Katibu umepokea mawasiliano yoyote au yapo njiani?

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba sijapokea maandishi. Kwa ajili hii nadhani ili tuwe na hakika kwa nafasi ile ambayo alikuwa anagombea ni vizuri tukatoa karatasi za kura.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza ni kweli jana mimi pamoja na Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Martha Umbullah tuliongea na mbele ya Mheshimiwa Umbullah, Mheshimiwa Sakaya aliamua kujitoa na asubuhi hii amenipa taarifa.

**SPIKA:** Pia nitoe taarifa tu kwamba nadhani Mheshimiwa Susan Lyimo umeacha kusema kwamba na Naibu Spika alikuwepo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Spika, hapa ni mahali ambapo ni wazi na kama ingekuwa ni kimya kimya ingekuwa ni sahihi kwamba ni lazima tuwe na maandiko. Lakini tumeuambia umma na tumetoa kwa *consituency* na hakuna upinzani kwa suala hilo. Kwa hiyo, nadhani taarifa iliyotolewa hapa ni halali.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA**: Mheshimiwa Spika, mimi ni Naibu Kiongozi wa Upinzani na kwa kawaida katika Kambi yetu kunapofanyika kitu sisi tunaulizwa kama viongozi. Mimi na mwenzangu Mheshimiwa Hamad Rashid tumeulizwa na wenzetu waliokuwa wagombea katika nafasi hii tufanye nini. Sisi tumeona katika nafasi hii hatuna sababu ya wanawake wetu na wanawake wa CCM kugombana kwa sababu katika hili tunacholenga ni uwakilishi wa akina mama. Kwa hiyo, kwa niaba ya Mheshimiwa Sakaya nathibitisha kwamba alijitoa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jambo hili halistahili mjadala mrefu. Tukiendelea tutakuwa tunatumia muda wa Bunge vibaya. Kwa hiyo, tuendelee. Katibu uwataje, sasa hakuna mahali popote penye ushindani, au sivyo? Nimeelewa hivyo! Hakuna. Basi nitawataja, anayetamkwa aje mbele tumwone, halafu basi tunamkubali.

**CHUO KIKUU CHA SAYANSI YA AFYA MUHIMBILI**

**SPIKA:** Mheshimiwa Rwilomba anawakilishwa na Mheshimiwa Nyawazwa, labda uje hapa. Nitangulie kusema tu kwamba uhusiano wao ni kwamba wanatoka Mkoa wa Mwanza, ni jirani yake, maana wale mnaojua kupepeta tena msije mkaanza ooh imekuwaje mwanamke anamwakilisha mwaume! Basi Mheshimiwa Nyawazwa unaweza kutoa utangulizi, mwenzetu yuko wapi na shukrani zake uzitoe. *(Kicheko)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mbunge wa Jimbo la Busanda, Wilaya ya Geita, naomba nichukue nafasi hii kuwaeleza kwamba ameondoka jana kwenda Muhimbili.

Kama mnavyojua Waheshimiwa Wabunge, kuna wakati alikuwa amelazwa Muhimbili, kwa hiyo, amekwenda kwa ajili ya *check-up* ya afya yake. Kwa niaba yake naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wabunge wote kwa kupitisha jina lake ili atuwakilishe katika Chuo Kikuu kile cha Muhimbili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana! Msalimie sana. Tunamtakia afueni kwa haraka.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru kwamba mmekubali tupite bila kupigiwa kura kwa sababu nayo hata kama ni NDIYO na HAPANA, HAPANA inamletea mtu *pressure* pia. Naomba niseme asante.

Ninaahidi kwamba, mimi kama Daktari niliyesoma Muhimbili nitakwenda kufanya kazi nzuri kuhakikisha kwamba vijana wanasoma, tunapata Madaktari wazuri na migomo inapungua. Naomba niseme asanteni sana! *(Makofi)*

**CHUO KIKUU CHA MZUMBE**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Magdalena Sakaya ambaye ameamua kujitoa na kunipa mimi fursa ya kuwa Mgombea wa Ujumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Mzumbe. Namshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, pili, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kupitisha jina langu, kwa kuniamini kwamba nitaliwakilisha vizuri Bunge lako Tukufu. Naahidi kabisa kwamba ninao uzoefu, nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu na kadri nitakavyowezeshwa na Mwenyezi Mungu kuliwakilisha Bunge lako Tukufu. Napenda kusema asanteni sana, nashukuru sana kwa heshima hiyo niliyopewa. Asante sana! *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana, Mheshimiwa Martha Umbulla!

**CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO**

**MHE. DR. OMARI M. NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa heshima na taadhima, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Wabunge wote, kwanza kwa kunipa kura nyingi katika kipindi kilichopita na zilikuwa za kishindo, na kwa bahati nzuri kipindi hiki sikupata mpinzani na wenzangu wakijua kwamba Chuo cha Sokoine kipo ndani ya Jimbo langu mimi. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa kuzingatia hilo na naahidi kwamba nitawawakilisha vizuri bila matatizo yoyote. Asanteni sana! *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Dr. Mzeru!

**CHUO KIKUU CHA DODOMA**

**MHE. JOB. Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa niaba yangu mwenyewe, kwa niaba ya Wabunge wa Mkoa wa Dodoma na wananchi wa Mkoa wa Dodoma kwa ujumla, tunawashukuru sana kwa nafasi hii ambayo mmeniamini niwalikilishe Bunge letu katika Baraza la Chuo Kikuu cha Dodoma. Kama mnavyojua, Waheshimiwa Wabunge, Serikali ya Awamu ya Nne imedhamiria kujenga Chuo kikubwa kuliko vyote hapa Dodoma. Nawahakikishia uwakilishi mwema na uliotukuka. Asanteni sana! *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Ndugai!

**CHUO KIKUU CHA ARDHI**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, awali ya yote napenda kutoa shukrani za dhati hasa kwa Wabunge wa CCM kwa kuweza kuniachia nafasi hii mimi Mpinzani ili niweze kuigombea. Kwa kweli nilikuwa najua nitapata mpinzani. Lakini nashukuru, naona ni imani kubwa mmenipa.

Na mimi naahidi kwamba kwa sababu mwaka uliopita mliweza kunichagua kuwawakilisha katika Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nadhani sasa mmeona kwa uwezo wangu basi niendelee kuwawakilisha katika katika Chuo Kikuu cha Ardhi.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na naahidi kwamba nitaendeleza juhudi zangu na nitashirikiana na ninyi kwa yote yale. Asanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Susan!

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naomba nitoe shukrani za dhati kwa nafasi mliyonipa ili niweze kuwawakilisha kwenye Bodi ya Chuo Kikuu cha Ardhi. Nawahakikishia Wabunge wenzangu, nitafanya kazi hiyo mliyonituma kwa bidii na nitawaletea kilicho bora. Asanteni sana!

**SPIKA:** Asante sana! Katibu tumemaliza?

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, tumefikia mwisho wa zoezi hili la kuchagua Wabunge watakaowakilisha Bunge hili katika Vyuo Vikuu vya Sayansi ya Afya Muhimbili, Chuo Kikuu cha Mzumbe...!

**SPIKA:** Wataje sasa!

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, wawakilishi wa Bunge hili kwa Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili ni Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba na Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya. Chuo Kikuu cha Mzumbe ni Mheshimiwa Martha J. Umbulla.

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ni Mheshimiwa Dr. Omar M. Nibuka. Chuo Kikuu cha Dodoma ni Mheshimiwa Job Y. Ndugai, na Chuo Kikuu cha Ardhi ni Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo na Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro. Naomba kusema kwamba hapa ndio mwisho wa zoezi hili la shughuli ya uchaguzi.

**SPIKA:** Asante sana! Sasa Waheshimiwa Wabunge, imebakia hoja moja tu ambayo hutolewa wakati huu. Lakini, kabla sijamwita mtoa hoja, napenda mtambue kuwepo kwenye *Speaker's Gallery*, Mheshimiwa Mama Regina Lowassa na kuwepo pia yule rafiki yangu wa kawaida anayeitwa Richard Lowassa – Spika mtarajiwa wa mwaka 2035, kwa maana hiyo hanipi ushindani wowote.

Kwa hiyo, mimi napenda nimsaidie tu kumpa *tuition* ili takapoiva wakati huo basi awe ni Spika madhubuti kuliko waliomtangulia. Baada ya kusema hayo na kwa heshima zote, sasa naomba kumwita Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe hoja ya kuliahirisha Bunge.

## HOJA YA KULIAHIRISHA BUNGE

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutulinda hadi siku ya leo tunapohitimisha Mkutano wa Nane wa Bunge lako Tukufu ulioanza rasmi tarehe 12 Juni, 2007. Huu ni muda wa takriban siku 67. Hongereni kwa kazi! Katika Mkutano huu hati 17 ziliwasilishwa mezani na Serikali ilijibu maswali 436 ya msingi yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wabunge na mengine mengi ya nyongeza. Aidha, Waheshimiwa Wabunge walijadili na kupitisha miswada mitatu (3).

Mheshimiwa Spika, lakini kabla ya kuendelea, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza sana Dr. Christine Ishengoma kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum. Nampongeza na kumkaribisha hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwa masikitiko makubwa kutoa rambirambi zangu kwako wewe Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote, kwa familia, ndugu jamaa na marafiki, kwa msiba wa mzee wetu, Chifu Abdallah Said Fundikira.

Marehemu Mzee Abdallah Fundikira amekuwa kiongozi wetu kabla na baada ya nchi yetu kupata uhuru. Wengi wetu tutakumbuka busara na hekima zake. Aidha, natoa pole kwa Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kufiwa na baba yake mzazi. Wazee wetu wote bado tuliwahitaji sana, lakini Mwenyezi Mungu amekubali watutangulie mbele za haki. Tunawaombea Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi Amina!

Mheshimiwa Spika, Bunge hili lilijadili kwa kina Miswada ifuatayo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2007 (*Finance Bill 2007*). Muswada huu ulilenga katika kuongeza, kukusanya mapato ya ndani na kuhamasisha wananchi kulipa kodi kwa hiari;

(ii) Muswada wa Sheria ya Matumizi wa Mwaka 2007(*Appropriation Bill 2007*). Kupitishwa kwa muswada huu kunatuwezesha kutumia fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ili kutekeleza yale yote tuliyoyakubali katika bajeti yetu;

(iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Bodi ya Elimu ya Juu. Muswada huu ulifanya mabadiliko katika vifungu mbalimbali vya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ya mwaka 2004 ili iweze kutekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Bunge lilifanya uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza katika Vyuo Vikuu kama ifyuatavyo:- Chuo Kikuu cha Sayansi ya Afya Muhimbili alichaguliwa Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba na Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Chuo Kikuu cha Mzumbe alichaguliwa Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine alichaguliwa Mheshimiwa Dr. Omar M. Nibuka.

Chuo Kikuu cha Dodoma alichaguliwa Mheshimiwa Job Ndugai na Chuo Kikuu cha Ardhi, alichaguliwa Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Aloyce Kimaro. Napenda kuwapongeza sana kwa kuchaguliwa kuliwakilisha Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkutano huu tunaohitimisha leo ni Mkutano wetu wa pili wa Bunge la Bajeti tangu tuchaguliwe kuwawakilisha wananchi kama Wabunge. Aidha, Mkutano huu umefanyika wakati tunakaribia kukamilisha nusu ya muda wetu hapa Bungeni kabla ya kufanyika kwa uchaguzi Mkuu mwingine mwaka 2010 ambao utatupima utendaji na ufanisi wetu katika kuwatumikia wananchi.

Katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge wamejadili na kupitisha bajeti ya Serikali ambayo itatekelezwa kwa kipindi cha mwaka 2007/2008. Bajeti hii imelenga kukusanya mapato ya ndani ya jumla ya shilingi trilioni 3.5 sawa na asilimia 18.1 ya Pato la Taifa. Kupatikana kwa makusanyo hayo kutaiwezesha Serikali kutekeleza mipango yake ya maendeleo kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, wakati nikihitimisha hoja ya makadirio ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu nilieleza Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ya Awamu ya Nne ipo makini kutekeleza ahadi zake, na kwamba *we are on time, we are on track, we are on the right direction* na tuko makini! Nilieleza kuwa ndege sasa iko tayari kupaa. Napenda tena kukariri kuwa mafanikio yaliyopatikana ni dhahiri. Wananchi waliotupigia kura wanayaona. Jumuiya ya Kimataifa imeona na kutoa pongezi.

Mheshimiwa Spika, lakini, wapo waliohoji kauli yangu na kueleza kuwa kupaa ninakokuzungumzia hakuna ukweli. Tena wakanichora kwenye magazeti katika katuni, nikiwa kwenye ndege huko juu peke yangu na nimewaacha wananchi huku chini.

Sote sisi ni mashahidi wa matatizo tuliyokumbana nayo katika muda mfupi. Matatizo hayo ni yale ya ukame, kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia, na mlipuko wa magonjwa ya binadamu na wanyama. Napenda tena nikariri hoja yangu kwa kueleza kuwa uzoefu wa Tanzania katika kusimamia mageuzi ya kiuchumi ni wa kuridhisha na kupigiwa mfano katika nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Spika, mara kwa mara tukitoa takwimu na taarifa tunaambiwa haziaminiki na tunaambiwa sio kweli. Sasa, hebu tusikie maelezo ya Shirika la Fedha Duniani. Mwezi Novemba, 2006 Shirika la Fedha Duniani *(IMF)* lilitoa taarifa kwamba Tanzania ni moja ya nchi za Afrika zenye sifa ya kusimamia kikamilifu sera zake za uchumi na imefanikiwa kutengemaza uchumi wake na pia ina mikakati mizuri ya kupunguza umaskini.

Nchi nyingine zilizokuwa na sifa hizo ni Nigeria, Uganda na *Cape Verde.* Chini ya mpango huo, Tanzania imefuzu vigezo vyote vya kuaminiwa na jumuiya ya kimataifa kuainisha masuala yake muhimu, kupanga vipaumbele na kusimamia utekelezaji wake yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na Taarifa ya Julai, 2007 ya *IMF*, katika miaka saba iliyopita, uchumi wetu umekua kwa wastani wa asilimia 6.3. Ukuaji huu umeelezewa kuwa ni moja ya viwango vikubwa vya ukuaji wa uchumi katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hili limetokana na sera nzuri za mageuzi ya uchumi ambao Serikali ya CCM imekuwa ikitekeleza. Mashirika ya Fedha ya Kimataifa likiwemo *IMF* yamekubali kuwa mageuzi ya Tanzania sasa yamekomaa.

Hali hii ndiyo inayotuwezesha kuhimili matatizo makubwa tuliyokumbana nayo katika muda mfupi huu. Katika mwaka huu wa fedha, Serikali itaendelea kutekeleza mageuzi haya ya kisera na kimiundo ili kuboresha maisha ya Watanzania. Serikali pia itajikita zaidi katika kuimarisha miundombinu na kuzidi kuimarisha mazingira ya kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nguzo kuu ya Serikali yoyote ile ni kodi. Serikali legelege haiwezi kukusanya kodi. Serikali inayokumbatia rushwa haiwezi kukusanya kodi. Uwezo wetu wa kukusanya kodi unaonekana dhahiri. Ukusanyaji wa mapato umeongezeka kuliko kipindi chochote katika historia ya nchi yetu. Tumeweza kukusanya mapato ya ndani ya jumla ya shilingi trilion 2.7 na hivyo kuvuka kiwango cha kukusanya mapato cha mwaka wa fedha 2006/07 kwa asilimia 11.3.

Mwezi uliopita, yaani mwezi Julai mwaka huu, Mamlaka ya Mapato Tanzania imeweza kukusanya jumla ya shilingi bilioni 248.4 na hivyo kuvuka lengo lililowekwa kwa mwezi huo la shilingi bilioni 245.9 kwa asilimia 1.1. Hii ni dalili nzuri kuwa tupo makini katika kuweka malengo yetu na tupo makini katika usimamizi na ukusanyaji wa mapato yatakayotuwezesha kutekeleza yale tuliyoahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tuendelee kudai na kukusanya kodi. Lazima tuendelee kutafuta vyanzo vipya vya kodi bila kuonea mtu na bila ya kuathiri kasi ya kukua kwa

uchumi wa taifa. Serikali zote duniani zinaendeshwa kwa kodi za wananchi; sembuse ya kwetu inayotegemea misaada ambayo chanzo chake ni kodi za wananchi wa nchi tajiri. Na kulipa kodi si kitu cha kufurahisha, japo ni cha lazima.

Ipo hadithi ya watu wawili, mmoja raia wa Uholanzi na mwingine raia wa Marekani waliokuwa wanazungumzia nchi zao. Mdachi akawa anamweleza Mmarekani maana ya rangi nyekundu, nyeupe na bluu zilizoko kwenye bendera ya Uholanzi. “Unajua bwana”, akaanza, “rangi za bendera yetu ni kielelezo cha kodi zetu. Nyuso zetu zinakuwa nyekundu tunapozungumzia kodi, zinakuwa nyeupe tunapoletewa madai ya kodi, na zinakuwa za bluu tunapolipa kodi.” Mmarekani akajibu. “Kumbe nyie ni kama sisi tu. Tena sisi tunaona nyota vilevile!” *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na kujua kuwa kulipa kodi si harusi, bado tuna kila sababu ya kujivunia mafanikio ya kukusanya kodi. Hatimaye lengo letu ni kuondokana na utegemezi kwa kodi za nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuupongeza uongozi na wafanyakazi wa *TRA* kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kuongezeka kwa mapato ndiko kulikowezesha Serikali kukabiliana na matatizo ya umeme kulikosababishwa na hali ya ukame, kugharamia miradi ya dharura ya upungufu wa chakula na mlipuko wa ugonjwa wa *RVF*. Kwa kuweka mipango thabiti, tunaongeza malengo, kupanua wigo wa kodi, na kuimarisha usimamizi na udhibiti ikiwa ni pamoja na kuziba mianya ya wakwepa kodi. Hatua hizi ndizo zinazotupa uwezo wa kupanga ongezeko la mapato ya ndani katika bajeti ya mwaka 2007/2008 hadi kufikia shilingi trilioni 3.5 sawa na ongezeko la asilimia 30 na hivyo kuwezesha kupunguza utegemezi kutoka asilimia 46 mwaka uliopita hadi asilimia 42 mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri basi kuwa tumeweka mazingira mazuri ya kujenga uchumi imara na unaokua. Pamoja na hatua hizo Serikali inapitia mpango wa awamu ya pili ya marekebisho ya sekta ya fedha ili iweze kuongeza mchango wake katika kukuza Pato la Taifa. Katika hili, sheria na kanuni za kukopesha na kukodisha vifaa vya ujenzi (*leasing*) zitawekwa ili wananchi wenye uwezo waweze kufanya hivyo. Aidha, karadha za nyumba *(mortgage finance)* nazo zitaanzishwa ili wananchi waweze kujenga makazi bora. Tunategemea kuleta miswada ya sheria hizo mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vile hii ni Serikali iliyowekwa madarakani na Chama chenye malengo, Chama chenye dira, Chama kilichojizatiti kusimamia utekelezaji wa ahadi zake, katika mwaka 2007/2008, tumeweka vipaumbele ambavyo vitaongeza kasi zaidi ya ndege yetu kupaa. Tumeamua kuwekeza katika elimu asilimia 18 ya bajeti ili kujenga taifa lenye watalaamu. Tunajenga miundombinu ambako tumewekeza asilimia 12.8 ya bajeti ili tuweze kuunganisha mikoa yote na kuibua uchumi vijijini. Tutaboresha huduma za afya kwa kuwekeza katika afya asilimia 10 ya bajeti na tutaendeleza kilimo asilimia 6.2 ya bajeti ili tuweze kujitosheleza kwa chakula na kuuza ziada nje ya nchi. Yote haya ni katika kupiga vita umaskini na kuleta maisha bora kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika siku 35 tulizojadili Bajeti ya Serikali na makadirio ya matumizi ya Wizara na taasisi za Serikali, kila waziri amejitahidi kuonyesha kuwa tunaposema tunapiga hatua, tunaposema tunapaa, tunaposema tupo makini na hatujapotea dira tuna maana gani. Napenda nitume fursa hii kwa muhtasari kudhihirisha hoja yangu kwa mifano michache. Wale Wapinzani wetu hupenda sana kutukosoa lakini naomba watukosoe kwa takwimu.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wakazi waishio vijijini umeongezeka kutoka asilimia 53.7 mwaka 2005/2006 hadi asilimia 55.7 mwaka 2006/2007 ikiwa ni ongezeko la asilimia 2. Ongezeko hili ni la kuridhisha na linaendana na lengo la MKUKUTA la asilimia 2 kila mwaka na lengo la Ilani ya Uchaguzi ya CCM la kufikia asilimia 65 ya wananchi waishio vijijini ifikapo 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa maji safi na salama kwa wakazi wa mijini katika Makao Makuu ya Mikoa 19 umeongezeka kwa asilimia 4.0 kutoka asilimia 74 mwaka 2005/2006 hadi asimia 78 mwaka 2006/2007. Ongezeko hili ni la kuridhisha na ni la juu ya lengo la wastani wa ongezeko la asilimia 3.2 mijini kila mwaka la MKUKUTA. Ongezeko hili pia linaendana na lengo la Ilani ya Uchaguzi ya CCM la kufikia asilimia 90 ya wananchi waishio mijini ifikapo 2010. Aidha, upotevu wa maji mijini ulipungua kutoka asilimia 41 mwaka 2005/2006 hadi asilimia 39 mwaka huu wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, vijiji 2,668 vilipimwa nchini. Hii ni sawa na asilimia 43 ya vijiji 6,219 vilivyokuwa vimepiwa tangu uhuru hadi 2005/2006. Vyeti vya ardhi ya vijiji vilivyotolewa vimeongezeka kutoka vyeti 191 mwaka 2005/2006 hadi kufikia 402 mwaka 2007/2007. Hatimiliki za kimila zilizotolewa zimeongezeka kutoka 2,062 mwaka 2005/2006 hadi 5,202 mwaka 2006/2007 sawa na ongezeko la asilimia 76 kwa mwaka mmoja. Nani anasema ndege haipai? Aidha, katika mwaka 2007/2007 mabaraza 10 ya ardhi yameundwa na kufanya jumla ya mabaraza yaliyopo kuwa 33. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imetambua miliki 230,000 za ardhi na nyumba kwenye maeneo yaliyojengwa kiholela. Leseni za makazi 75,000 zimetolewa hadi kufikia Juni, 2007. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 19.8 za kodi ya pango la Nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa zikikusanywa mwaka 2006/2007 ikilinganishwa na Shilingi 14.4 zilizokusanywa mwaka 2004/2005. Mapato haya yameliwezesha Shirika kujenga nyumba za kuuza na kukodi katika miji ya Dar es Salaam, Arusha Mjini, Chalinze – Pwani, Ruangwa, Dodoma, Iringa, Shinyanga na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliongeza kiwango cha ruzuku ya mbolea kutoka tani 63,000 mwaka 2005/2006 hadi tani 89,942 mwaka 2006/2007 sawa na ongezeko la asilimia 42.8. Aidha, katika mwaka 2007/2008 tunatarajia kusambaza mbolea tani 98,760. Ongezeko la matumizi ya mbolea nchini pamoja na mambo mengine limesababisha uzalishaji wa mazao mbalimbali kuongezeka. Kwa mfano, kwa mazao ya biashara, kati ya mwaka 2005/2006 na 2006/2007 uzalishaji uliongezeka kama ifuatavyo: (a) Kahawa kutoka tani 34,334 hadi tani 48,869; (b)Tumbaku kutoka tani 56,463 hadi

tani 65,299; (c) Chai kutoka tani 30,000 hadi tani 34,446; (d) Mkonge kutoka tani 27,794 hadi tani 30,934; na (e) Korosho kutoka tani 77,158 hadi tani 92,232. Nani anasema ndege haipai?

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa uzalishaji ni ishara nzuri kwamba wakulima wetu sasa watauza zaidi na hivyo kuongeza kipato chao. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 83.4 zilizotengwa chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *(ASDP)* kitasaidia kuwawezesha wakulima kupata mafunzo na teknolojia za kilimo pamoja na kuwa na uhakika wa masoko na miundombinu.

Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali itaajiri watumishi 2,500 wa kilimo na mifugo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango huu. Vyote hivi vitasaidia kuwawezesha wakulima kuongeza tija, mavuno, mapato na faida katika kilimo maradufu. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wakulima wote kwa juhudi walizofanya katika mazao haya.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao ya chakula nao umeongezeka kutoka tani milioni 10.9 mwaka 2005/2006 na kufikia tani milioni 11.02 mwaka 2006/2007. Kutokana na ongezeko hilo, katika mwaka 2006/2007 Taifa lilijitosheleza kwa chakula kwa asilimia 112 ikilinganishwa na mahitaji yaliyokuwepo ya tani milioni 9.75. Katika mwaka 2007/2008 inatarajiwa kuwa tutajitosheleza kwa chakula kwa asilimia 109 ikilinganishwa mahitaji ya tani milioni 10.09. Aidha, Hifadhi ya Chakula ya Taifa imeimarika kutoka tani 6,570 mwezi Juni, 2006 hadi kufikia tani 128,668 mwezi Juni, 2007. Hali hii inadhihirisha kuwa tumejiandaa kukabiliana na majanga ya upungufu wa chakula endapo yatajitokeza.

Kuhusu elimu ya msingi, idadi ya wanafunzi katika shule za msingi imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 6.7 kwa mwaka tangu mwaka 2003 hadi 2007 ikilinganishwa na wastani wa ongezeko la watu la asilimia 2.9 kwa mwaka. Kiwango cha kufaulu elimu ya msingi kimeongezeka kutoka asilimia 27.1 mwaka 2002 hadi asilimia 70.5 mwaka 2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiwango hicho kinaonesha ubora wa elimu tunayotoa kwa vijana wetu. Jambo lingine la kujivunia ni kuwa wanafunzi waliofanya vizuri wengi wao wametoka katika shule za msingi za kawaida kabisa wala sio zile zinazoitwa *International* wala *Academy*. Nitatoa mfano, kwa wavulana, mwanafunzi Seifu R. Mwingiliko aliyeshika nafasi ya kwanza Kitaifa katika mtihani wa darasa la saba mwaka 2006 alipata alama 230 kati ya 250. Mwanafunzi huyu alitoka shule ya msingi Mapinduzi, Wilaya ya Rufiji kwa Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia. Hongera sana Profesa. *(Makofi)*

Mwanafunzi Shadrack M. Wilson alishika nafasi ya pili kwa kupata alama 229 na alitoka shule ya msingi Mapinduzi - Serengeti, hongera Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, mwanafunzi Godfrey Sally aliyeshika nafasi ya tatu kwa kupata alama 229 alitoka shule ya msingi *Rocken Hill* - Kahama, Shinyanga. Hongera Mheshimiwa

Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Ezekiel Maige na Mheshimiwa James Lembeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wasichana, mwanafunzi Paulina Raphael aliyeshika nafasi ya kwanza kwa kupata alama 228 alitoka shule ya msingi Kashishi - Kahama, Shinyanga. Azida A. Hassan aliyeshika nafasi ya pili kwa kupata alama 226 alitoka shule ya msingi Mvumi Misheni – Dodoma Vijijini nyumbani kwa Mheshimiwa John Malecela. Hongera sana Mheshimiwa John Malecela. *(Makofi)*

Mwanafunzi Janeth J. Ayubu aliyeshika nafasi ya tatu alitokea shule ya msingi Kwesasu – Same, Kilimanjaro kwa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Dr. Mathayo David Mathayo, shule zote hizi ni za vijijini. Vijana hawa wametuthibitishia kuwa elimu yetu bado ni bora na kinachohitajiwa ni kuondoa vikwazo vichache vilivyopo, kuboresha huduma muhimu na kuendelea kuajiri walimu wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimelazimika kusema hili kwa kuwa kumekuwepo na imani potofu miongoni mwa baadhi ya Watanzania kuwa elimu inayotolewa katika shule za vijijini au zile za kawaida ni duni. Matokeo haya yanaonyesha kuwa juhudi zetu za kuimarisha mazingira ya kufundishia na kupeleka walimu zinatoa matunda mazuri. Ubora wa elimu inayotolewa unaonekana. Natoa wito kwa wanafunzi wote kusoma kwa bidii na kuachana na maelezo yanayotolewa ya kuwakatisha tamaa katika masomo yao. Wanafunzi wote wa Tanzania wajiulize kama wenzao hawa ambao wanasoma shule za kawaida kabisa wameweza kufanya vizuri kwa nini isiwe wao?

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana wanafunzi hawa kwa kuwaonesha wanafunzi wengine kwamba kila kitu kinawezekana kama kuna nia na juhudi. Nawapongeza pia walimu wao kwa kazi nzuri waliyoifanya. Nawapongeza Wabunge kwa kusimamia vizuri elimu katika Majimbo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya sekondari, kwa upande wa elimu ya sekondari idadi ya wanafunzi waliojiunga kidato cha kwanza imeongezeka kwa asilimia 65 kutoka wanafunzi 243,359 mwaka 2006 hadi wanafunzi 401,011 mwaka 2007. Aidha, wanafunzi waliojiunga na kidato cha tano waliongezeka kwa asilimia 17.4 kutoka wanafunzi 15,509 mwaka 2005 hadi 18,211 mwaka 2006. Idadi ya wanafunzi wa sekondari (kidato cha kwanza hadi cha sita) imeongezeka kwa asilimia 51 kutoka 675,672 mwaka 2006 hadi 1,020,510 mwaka 2007. Ongezeko hilo linachangiwa kwa kiasi kikubwa na ongezeko la asilimia 69 la wanafunzi katika shule za sekondari za Serikali kutoka wanafunzi 490,492 mwaka 2006 hadi 829,094 mwaka 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 idadi ya madarasa mapya yaliyojengwa ya sekondari zenye kidato cha kwanza hadi cha nne ni 1,631 na yaliyojengwa kwenye sekondari zenye kidato cha tano na sita ni 128. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwango vya kufaulu katika ngazi ya sekondari, kiwango cha kufaulu kwa kidato cha pili kimeongezeka kutoka asilimia 71.6 mwaka

2002 hadi asilimia 76.3 mwaka 2006. Aidha, kiwango cha kufaulu kidato cha nne kimeongezeka kutoka asilimia 86.3 mwaka 2002 hadi asilimia 89.1 mwaka 2006. Kuwepo kwa kundi kubwa la Watanzania wenye elimu ya kidato cha nne kutaleta mabadiliko makubwa kwani tutakuwa na jamii iliyoelimika zaidi, jamii ambayo itakuwa inaweza kukabiliana na changamoto ya dunia hii ya sayansi na teknolojia. Lakini vile vile vijana hawa watakuwa chachu katika kubadili hali ya maisha vijijini. Tunachotakiwa kufanya ni kuendelea kuweka mazingira yatakayowawezesha kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya juu, Serikali imeongeza idadi ya wanafunzi katika elimu ya juu kutoka wanafunzi 52,108 mwaka 2005/2006 hadi kufikia wanafunzi 68,929 mwaka 2006/2007 ambalo ni ongezeko la asilimia 30.6. Tumeanzisha Vyuo Vikuu kamili vitatu vya umma mbavyo ni Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya cha Muhimbili *(Muhimbili University of Health and Allied Sciences – MUHAS)*, Chuo Kikuu cha Ardhi *(Ardhi University*) na Chuo Kikuu cha Dodoma *(University of Dodoma).* Uanzishwaji wa Vyuo Vikuu hivi unafanya Tanzania kuwa na jumla ya Vyuo Vikuu nane vya umma na Vyuo Vikuu Vishiriki vinne vya umma. Ongezeko hili la Vyuo Vikuu litatuwezesha kuchukua wanafunzi wengi wanaofaulu vizuri mitihani ya kidato cha sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu afya, Serikali imeongeza kiwango cha chanjo ya Surua kutoka asilimia 72 mwaka 2000 hadi asilimia 90 mwaka 2006. Aidha, matumizi ya Serikali katika kupambana na UKIMWI yameongezeka kutoka shilingi bilioni 26.4 mwaka 2004 hadi shilingi bilioni 42 mwaka 2006. Serikali kwa kushirikiana na wananchi imejenga zahanati 255 katika mwaka 2006/2007 ikiwa ni asilimia 39 ya vituo 652 vilivyoko nchini. Kama nilivyotangulia kusema Serikali imetenga asilimia 10 ya Bajeti nzima sawa na shilingi bilioni 590 kwa ajili ya sekta ya afya. Tengeo hili ni ongezeko la asilimia 38 ikilinganishwa na shilingi bilioni 427.4 zilizotengwa mwaka jana. Kati ya fedha zilizotengwa shilingi bilioni 18.1 ni kwa ajili ya kusomesha watumishi 6,450 wa afya nchini, ununuzi wa vifaa na dawa. Aidha, Serikali imeongeza udahili wa wanafunzi wa Shahada ya Udaktari kutoka 1,427 mwaka 2005/2006 hadi 1,772 mwaka 2007/2008. Lengo ni kufikia uwiano wa daktari mmoja kwa wananchi 10,000 kutoka uwiano wa sasa wa daktari mmoja kwa wananchi 25,000 ifikapo mwaka 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu utalii, idadi ya watalii walioingia nchini katika mwaka 2006 imeongezeka kwa asilimia 5.12 ikilinganishwa na mwaka 2005. Watalii hao waliliingizia Taifa jumla ya shilingi trilioni 1.08 ikilinganishwa na shilingi bilioni 929 zilizopatikana mwaka 2005 sawa na ongezeko la asilimia 14.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira na uwekezaji, katika mwaka 2006, ajira mpya 201,390 zilipatikana ikilinganishwa na lengo la wastani wa ajira 200,000 kwa mwaka la Ilani ya Uchaguzi ya CCM, huu ni mwanzo mzuri. Kwa hiyo, tupo kwenye malengo yetu. Kasi ya ukuaji wa ajira inatarajiwa kuongezeka baada ya Serikali kuanza kutoa mikopo kwa wajasiriamali kupitia Benki za *NMB* na *CRDB.* Katika mwaka 2006/2007, benki hizo zimetoa mikopo yenye jumla ya shilingi bilioni 25.74 kwa wajasiriamali 27,344. Utaratibu huu wa kutoa mikopo kwa wajasiriamali utaendelea katika mwaka 2007/2008. *(Makofi)*

Aidha, Serikali imeendelea kutoa mikopo kwa wajasiriamali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Vile vile, jumla ya miradi mipya 1,679 ya maendeleo yenye thamani ya shilingi bilioni 73.9 ilizinduliwa. Aidha, zipo asasi binafsi za fedha kama vile *Pride Tanzania, Easy Finance* na mabenki ambazo nazo zinatoa mikopo kwa wajasiriamali. Ni wazi kuwa juhudi zote hizi zitachochea ongezeko la ajira na hivyo ongezeko la ukuaji wa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezeshaji Halmashauri, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua umuhimu wa mamlaka za wananchi. Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, imeeleza wazi majukumu ya Serikali katika kuziimarisha mamlaka hizi. Vita dhidi ya umaskini, kubadilika kwa uchumi katika ngazi za chini, kutawezekana kwa kuelekeza rasilimali watu na fedha katika ngazi za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeonesha dhamira hiyo kwa vitendo. Ruzuku iliyotengwa kwa ajili ya Serikali za Mitaa imeongezeka kutoka shilingi bilioni 725.6 mwaka 2006/2007 hadi kufikia shilingi bilioni 1,084.1 mwaka 2007/2008. Hivyo, kuna ongezeko la asilimia 66. Changamoto kwetu sote ambao ni viongozi katika ngazi hizo ni kuhakikisha kuwa rasilimali hizi kweli zinatumika kuleta mabadiliko ya wananchi kwa kuboresha huduma mbalimbali. Waheshimiwa Wabunge, ninyi ni Madiwani fedha zinatumika katika Halmashauri ni wajibu wetu tukazisimamie ili zilenge wananchi waliokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya viwanda, kufuatia uhamasishaji wa sekta binafsi kati ya mwaka 2005 na Machi, 2007 jumla ya miradi ya viwanda 66 ilipewa leseni kati ya hiyo 48 tayari imeanza uzalishaji na kuajiri wafanyakazi 4,337. Utafiti katika mikoa 21 umebaini ongezeko la ajira katika sekta ya viwanda kutoka watu 88,7134 hadi watu 93,426 kati ya mwaka 2005 na 2006.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa viwanda vidogo, Serikali kupitia *SIDO*, ilitoa mafunzo ya uhunzi kwa vikundi 841, useketaji *(handloom weaving)* kwa wajasiriamli 100, usindikaji wa ngozi kwa vikundi 12 na mafunzo ya ujuzi wa uzalishaji mali kwa wajasiriamali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wajasiriamali wadogo *(NEDF)*. *(Makofi)*

Aidha, kiwango cha mikopo kimeongezeka toka shilingi 500,000 hadi shilingi 2,500,000 kwa miradi ya uzalishaji. Kwa waliopata fursa ya kutembelea Maonyesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam mwaka huu, mmejionea ubora wa bidhaa za wajasiriamali wa Kitanzania wanavyojidhatiti kukabiliana na changamoto za utandawazi. Huu ndio uwezeshaji tunaouzungumzia. Huku ndiko kuweka mazingira ya kukua kwa hali za maisha za watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madini mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuongezeka kwa mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Taifa hadi kufikia asilimia 3.8 mwaka 2006 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2005. Aidha, mauzo ya madini nje ya nchi yalifikia dola za Marekani milioni 856.8 mwaka 2006 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 711.3 mwaka 2005 sawa na ongezeko la asilimia 20.

(ii) Kuanza kulipwa kwa kodi ya Halmashauri *(Local government levy)* kwa kiasi cha dola za Marekani 200,000 kwa mwaka kwa kila Halmashauri ambako kampuni za madini zina migodi. Halmashauri hizo zinazonufaika na makubaliano hayo ni Tarime, Kahama, Nzega, Geita na Biharamulo. *(Makofi)*

(iii) Kukusanywa kwa maduhuli ya shilingi bilioni 51.3 ilipofika Juni 30, 2007 ikilinganishwa na makadirio ya shilingi bilioni 45.1 ambalo ni ongezeko la asilimia takriban 14. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara, kwa upande wa barabara za lami, Serikali imeweza kujenga barabara mpya za lami zenye urefu wa kilometa 318 kwa kipindi cha mwaka 2005/2006 na 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kulinganisha malengo haya na utekelezaji wa milenia, mafanikio haya ninayoyazungumzia yanapaswa vile vile kupimwa kwa kutumia vigezo vya vya milenia. Tanzania ni moja ya nchi ambazo zimepiga hatua katika utekelezaji wa baadhi ya malengo haya ikilinganishwa na nchi nyingine duniani. Tunayo mifano mizuri ya utekelezaji wa malengo hayo kama ifuatavyo:-

(i) Kwenye elimu, lengo ni kuhakikisha kwamba kila mtoto anayestahili kupata elimu ya msingi anapata nafasi ya kwenda na kumaliza shule ya msingi ifikapo mwaka 2015. Kwa Tanzania asilimia ya watoto wenye umri wa kwenda shule ya msingi (*Net Enrolment Ratio*) ilifikia asilimia 96 katika mwaka 2006 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 70 katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara na wastani wa asilimia 88 katika nchi zinazoendelea. Kiwango hicho kimepanda na kufikia asilimia 97.3 mwaka 2007. *(Makofi)*

(ii) Jinsia, lengo ni kuongeza usawa wa jinsia na katika shule za msingi na sekondari na nyanja mbalimbali za maisha ifikapo mwaka 2015. Nchini Tanzania, uwiano wa wanafunzi wa kike kwa wa kiume katika shule za msingi umeongezeka kutoka 1:1.05 mwaka 2003 hadi 1:1.03 mwaka 2007. Uwiano wa wanafunzi wa kike kwa wa kiume katika shule za sekondari nao umeongezeka kutoka 1:1.19 mwaka 2003 hadi 1:1.14 mwaka 2007 Uwakilishi wa wanawake katika Bunge nao umeongezeka kutoka asilimia 15 mwaka 1995 hadi asilimia 30 mwaka 2006. Najua sasa wanalenga asilimia 50 kwa 50. *(Makofi)*

(iii) Kupunguza vifo vya watoto, lengo ni kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano kwa asilimia 66 sawa na theluthi mbili kati ya mwaka 1990 na 2015. Taarifa za vigezo vya malengo ya milenia vilivyotolewa na Umoja wa Mataifa mwaka 2006 inaonesha kuwa katika mwaka 1990 vifo hivyo vilikuwa 161. Vifo hivyo

vilipungua hadi watoto 141 kwa kila watoto 1,000 mwaka 2000 na hadi watoto 112 mwaka 2004 sawa na punguzo la asilimia 30 tangu mwaka 1990 na asilimia 20 tangu mwaka 2000. Wastani kwa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara mwaka 2005 ulikuwa vifo 166 kwa watoto 1,000 waliozaliwa hai.

(iv) Kuboresha huduma za uzazi, lengo la milenia ni kupunguza kwa asilimia 75 vifo vya wanawake vitokanavyo na uzazi kati ya mwaka 1990 na 2015. Katika nchi yetu vifo hivyo vilikuwa 770 kati ya wanawake 100,000 waliojifungua mwaka 1990, vikaongezeka hadi 1,500 mwaka 2000 na kupungua hadi 578 mwaka 2004. Hii ni sawa na punguzo la asilimia 61 katika miaka minne tu. *(Makofi)*

(v) Kujenga ushirikiano wa maendeleo, itakumbukwa kuwa Tanzania ilikuwa miongoni mwa nchi za mwanzo kabisa kunufaika na msamaha wa madeni wa nchi maskini sana na zenye madeni makubwa duniani kupitia Mpango wa *HIPC*. Aidha, nchi yetu imekuwa pia kati ya miongoni mwa nchi za mwanzo kabisa ambazo zimekubaliwa na kunufaika na msamaha mkubwa wa madeni chini ya Benki ya Dunia *(WB),* Shirika la Fedha la Kimataifa na Benki ya Maendeleo ya Afrika kupitia Mpango wa *Multilateral Debt Relief Initiative (MDRI).* Pamoja na misamaha hii ya madeni, nchi yetu pia inanufaika na mipango mbalimbali ya masoko yasiyo na ushuru kama vile *AGOA, EBA, Canadian Initiative on duty free and quota free market access* na lile soko la Wachina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Utawala Bora na mapambano dhidi ya rushwa, Tanzania imekuwa nchi ya pili duniani katika kutekeleza masuala yanayohusu kupambana na rushwa. Taarifa ya Taasisi ya Benki ya Dunia *(World Bank Institute) World Wide Governance Indicators 1996 – 2006* inaonyesha kuwa katika kipindi cha miaka kumi iliyopita 1996 - 2006, Tanzania na nchi ya Serbia zimefanya vizuri katika mapambano dhidi ya rushwa kama moja ya vigezo muhimu katika kupima utekelezaji wa utawala bora.

Mheshimiwa Spika, aidha, utafiti umeonyesha kwamba Tanzania ni mojawapo ya nchi saba za Afrika zilizopiga hatua kubwa katika eneo la utawala bora. Nchi nyingine ni Niger, Sierra Leone, Angola, *DRC*, Liberia na Rwanda. Matokeo ya utafiti huo vile vile yanaonyesha kiwango cha ubora wa nchi husika ikilinganishwa na asilimia ya nchi nyingine zilizo chini yake katika kila kipengele. Uchambuzi unaonesha mafanikio ya kupita jumla ya wastani wa asilimia 41 ya nchi 212 duniani zilizojumuishwa katika utafiti huo. Mafanikio hayo kwa kuangalia kipengele kimoja kimoja ni kama ifuatavyo:-

(i) Katika kipengele cha kudhibiti rushwa, tumeruka kutoka nafasi ya 147 hadi 120 na kuzipita nchi 27. *(Makofi)*

(ii) Kuhusu utulivu wa kisiasa tumetoka nafasi ya 147 hadi 126 na kuzipita nchi 21.

(iii) Uwajibikaji na uhuru wa kutoa maoni tumevuka kutoka nafasi ya 139 mwaka 2004 hadi 126 mwaka 2006 kwa kuzipita nchi 13.

(iv) Kipengele cha uimara wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake tumesonga mbele kutoka nafasi ya 125 hadi nafasi ya 119 na kuzipita nchi 6. *(Makofi)*

(v) Kuhusu utawala wa sheria, Tanzania imefanikiwa kutoka katika nafasi ya 126 mwaka 2004 na kufika nafasi ya 121 mwaka 2006 na kuzipiku nchi 5. *(Makofi)*

(vi) Mwisho katika kipengele cha kiwango cha udhibiti wa ubora wa huduma zitolewazo kwa wananchi, tumetoka nafasi ya 133 hadi 131 na kuzipita nchi mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeamua kueleza haya ili Watanzania waelewe kuwa nchi yetu inapiga hatua na wale rafiki zangu wanaokataa kwamba ndege haipai basi wanipe wao takwimu tofauti na hizi. Maana iwe kwa vigezo vya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, iwe kwa vigezo vya MKUKUTA au vigezo vya Malengo ya Milenia nchi inasonga mbele. Ipo methali isemayo ni lazima umle tembo kipande kimoja kimoja kwa wakati na Mahatma Gandhi aliwahi kusema tofauti kati ya tunachokifanya na kile ambacho tunao uwezo wa kukifanya inaweza kutatua matatizo mengi ya dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeyaeleza haya yote ili tujue mafanikio haya, ili tuone hatua moja baada ya nyingine tunayopiga, ili tuone kuwa tunao uwezo mkubwa. Kwa hiyo, tusilegeze kamba, tuongeze juhudi zaidi, tusijidharau, tusibeze mafanikio hayo, lakini vile vile tusiache kukosoana pale tunapoona kuwa wapo wanaotuwekea vizuizi katika mbio zetu za maendeleo. Tusiwaonee haya wanaotuchelewesha. Ni lazima watupishe! Hii ni Serikali iliyodhamiria kwa vitendo kutekeleza yale yote yenye lengo la kuwawezesha wananchi kubadili maisha yao yawe ya neema zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta isiyo rasmi, kwa kutambua umuhimu wa kuongeza kasi ya kupanua fursa zitakazoongeza ajira, napenda nizungumzie kwa kifupi sekta isiyo rasmi. Serikali inatambua mchango mkubwa unaotolewa na sekta isiyo rasmi katika Pato la Taifa hasa kuongeza ajira na kipato kwa wananchi. Kama itakavyokumbukwa moja ya ahadi za Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ni kutoa ajira zaidi ya milioni moja ifikapo 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzoefu wa nchi nyingi duniani unaonyesha kuwa sekta isiyo rasmi, licha ya kuongeza ajira ina uwezo mkubwa katika nyanja mbalimbali kama vile:-

(i) Kuongeza uzalishaji wa bidhaa zinazozalishwa nchini kwa ajili ya soko la ndani na nje;

(ii) Kukuza ubunifu, teknolojia na vipaji vya wajasiriamali;

(iii) Kuongeza thamani ya mazao na bidhaa nyingine kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya usindikaji; na

(iv) Kuongeza kipato cha mwananchi.

Aidha, sekta isiyo rasmi ni hatua muhimu ya awali ya kuwajengea wananchi utamaduni wa ujasiriamali na kuthubutu kufanya biashara na kuwekeza na hii ndio fursa ya kuingia katika sekta rasmi ili kujenga sekta binafsi iliyo imara nchini. Hivyo, lazima sekta hii iimarishwe, isaidiwe na kuwekewa mazingira mazuri ya kisera na miongozo ya kuirasimisha kwa manufaa ya Taifa. Mamlaka za Serikali za Mitaa zina wajibu mkubwa katika kukuza sekta hii ili iingie katika mfumo rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu za utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi *Integrated Labour Force Survey* uliofanyika mwaka 2005/2006 zinaonyesha kukua haraka kwa sekta isiyo rasmi nchini. Kwa mfano, sekta isiyo rasmi ilikua kutoka asilimia 8.5 mwaka 2000/2001 mpaka asilimia 11.5 mwaka 2005/2006. Aidha, takwimu zinaonyesha kwamba sekta hii huchangia asilimia 40 ya Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa ya hivi karibuni iliyoandaliwa kupitia Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge (MKURABITA), inaeleza kuwa sekta isiyo rasmi katika biashara na rasilimali *(Informal Businesses and Properties)* inajumuisha asilimia 89 ya rasilimalli isiyohamishika na ina thamani ya zaidi ya dola za Kimarekani bilioni 29. Aidha, utafiti uliofanywa na Taasisi ya Benki ya Dunia *(The International Finance Company)* unaonyesha kuwa ziko kampuni za biashara ndogo takribani milioni 2.7 nchini. Sehemu kubwa ya kampuni hizi ambazo ni sawa na asilimia 98 ni kampuni za sekta isiyo rasmi. Vile vile taarifa inaonyesha kwamba takriban watu wapya 700,000 wanajiunga na soko la ajira kila mwaka. Kati ya hao, watu 500,000 wanakadiriwa kuwa ni wahitimu wa shule katika ngazi mbalimbali. Wengi wao hawana ujuzi unaouzika katika soko la ajira. Takwimu zinaonesha pia kuwa sekta ya umma inaajiri watu 40,000 tu ya wanaoingia katika soko la ajira kila mwaka hivyo kuacha watu 660,000 kujiunga na sekta isiyo rasmi. Kwa hali hii mchango wa sekta isiyo rasmi ni muhimu sana. Kwa kuzingatia mazingira ya nchi yetu, ni lazima kabisa tuchukue hatua thabiti za kuisaidia na kuikuza sekta hii. Mamlaka za Serikali za Mitaa, zisiione sekta isiyo rasmi kwa mtazamo hasi bali iweke mazingira yenye kuiwezesha kukua, kuimarika na hatimaye kujiunga na sekta rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kujikomboa kutoka katika umaskini, Serikali nyingi duniani zimeachana na utaratibu wa kuendelea na mpango wa kuwa mwajiri mkubwa katika nchi zao. Serikali hizo zinajitahidi kuiwezesha sekta binafsi ikiwemo sekta isiyo rasmi kuwa ndiyo yenye kutoa ajira kubwa nchini. Niruhusu nitoe uzoefu wa nchi chache mbili tu ya Thailand na jirani zetu wa Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Thailand, utafiti uliofanywa na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP)* nchini Thailand unaonyesha kuwa nchi hiyo ilifanikiwa kuinua sekta isiyo rasmi na kuiingiza katika sekta rasmi kwa kuweka sera nzuri za uchumi jumla na mazingira bora ya kuvutia uwekezaji wa ndani na nje. Aidha, wafanyabiashara wa ndani walithubutu na kuwa tayari kubeba hasara za kibiashara *(business risks),* kupenda kujiendeleza hasa kupata elimu ya ujasiriamali na ubunifu wao wa kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa jirani zetu Kenya, sekta isiyo rasmi inajulikana kwa jina maarufu kama Jua Kali. Aidha, Kenya wanao mpango maalumu unaojulikana kama *Small Enterprise Jua Kali Development in Kenya*. Lengo la mpango huo ni kukuza sekta hii iwe ni sekta kubwa yenye kutambulika katika kuchangia kwenye uchumi wa Taifa wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzoefu tunaoupata kwa nchi hizi za Thailand na Kenya ni kielelezo kwamba kwa kuweka sera na mipango mizuri, sisi pia tunao uwezo wa kufanya vizuri kama tutatumia sekta hii vizuri kwa maendeleo ya nchi yetu. Hii ni changamoto kubwa kwetu kutumia uzoefu huo kuingiza sekta isiyo rasmi kwenye mfumo rasmi ili ichangie zaidi kwenye uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizopo zinazoikabili sekta isiyo rasmi nchini ni pamoja na ukosefu wa mitaji ya kuanzisha au kuendeleza miradi yao, kutokidhi vigezo na masharti ya benki na asasi nyingine za kifedha ya kukopesheka kwa urahisi, ukosefu wa maeneo ya kufanyia kazi au kuwekeza, ukosefu wa ubunifu na teknolojia duni. Watu wengi katika sekta isiyo rasmi wanaiga na kuanzisha biashara ya aina moja, jambo ambalo linawaathiri kibiashara, miundombinu duni ya masoko na mawasiliano hafifu hasa vijijini, wajasiriamali wengi kushindwa kumudu gharama za mafunzo ya kuongeza ujuzi wa kuendeleza biashara zao, ubora hafifu wa bidhaa zitokanazo na sekta isiyo rasmi na kutokuwa na ushirikiano imara kati yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa sekta isiyo rasmi kwenye mchango wa uchumi wa Taifa hasa katika uzalishaji, ufundi na biashara. Vile vile, Serikali inatambua wajasiriamali wadogo wadogo wenye viwanda vyao vidogo na ambao wanatoa huduma muhimu sana kwa umma. Hatua zimeanza kuchukuliwa za kurasimisha mali na biashara za sekta isiyo rasmi ili kuwarahisishia wajasiriamali wadogo kuwa na dhamana za kuwawezesha kupata mikopo kutoka mabenki kwa ajili ya kuanzisha biashara mpya na kupanua za zamani.

Mheshimiwa Spika, aidha, wajasiriamali hawa wadogo wanapatiwa elimu, kuwawezesha kuungana na kuunda umoja wenye nguvu, kuwatafutia masoko na kadhalika. Chini ya Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), hatua zinachukuliwa za kurasimisha mali na biashara za sekta isiyo rasmi. Hii itawarahisishia wajasiriamali wadogo kuwa na dhamana za kuwawezesha kupata mikopo kutoka mabenki, kuanzisha biashara mpya na kupanua za zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali vile vile inatekeleza Mkakati wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA). Lengo la Mkakati huo ni kuandaa mfumo wa Kitaifa wa kumiliki mali na uendeshaji biashara utakaoainisha na kuboresha kanuni na taratibu zinazotumiwa na makundi mbalimbali nchini na kuwa mfumo mmoja wa kisheria. Hii itafanya walengwa waweze kuutumia mfumo huo kupata mitaji ya kugharamia shughuli zao kadri ya utashi wao na kufanya biashara katika mazingira bora zaidi. Hadi sasa kuna marekebisho mbalimbali yanayoendelea katika sekta nyinginezo hasa sekta ya ardhi na makazi, sheria na biashara na masoko. Mifuko mbalimbali

imeanzishwa ili kuendeleza biashara na viwanda vidogo na vya kati. Mojawapo ya mifuko hiyo ni *National Entrepreneurship Development Fund – NEDF* inayosimamiwa na *SIDO*.

Mheshimiwa Spika, katika kuiendeleza sekta hii yapo majukumu ya wadau mbalimbali. Wadau wa awali kabisa ni Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mamlaka hizi zinao wajibu wa kuisaidia sekta hii kwa kutenga maeneo rasmi ya kufanyia kazi. Katika miji yetu hivi sasa tunapima viwanja vingi kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Tunao wajibu wa kuhakikisha kuwa tunaitambua sekta hii na kutenga maeneo kwa ajili yao na kwa ajili ya viwanda vidogo. Wadau wengine ni wajasiriamali wenyewe. Wito wangu kwao ni kuwa waheshimu sheria na taratibu ili mamlaka husika ziweze kuwasaidia. Zipo pia taasisi za fedha ambazo kutokana na kuimarika kwa uchumi na hatua tunazochukua za kurasimisha mali za wajasiriamali wadogo, waone sasa wanavyoweza kuingia katika sekta hii na kuisaidia ipate mtaji wa kuiwezesha kupanuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba tunayo nafasi ya kuitumia sekta hii isiyo rasmi kufanya mambo makubwa ambayo yatasaidia nchi yetu kusonga mbele kimaendeleo. Sekta hii inaweza kabisa kuwa mkombozi wa wengi. Jambo la kujiuliza ni kwamba kama nafasi kama hizo zipo kwa nini hazitumiki vizuri? Tatizo ni nini? Kwa nini maeneo ya vijijini bado ndiyo yamebakia nyuma pamoja na nafasi tulizo nazo? Serikali kwa upande wake itaendelea kuweka mazingira mazuri na sera zitakazowezesha sekta binafsi na isiyo rasmi kukua na kukubalika ili kutoa ajira nyingi zaidi na kuchangia zaidi katika Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 ilimnukuu Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa akiwa Mwenyekiti wa CCM tarehe 25 Agosti, 2004 akisema, namnukuu: “Uchumi wa soko hauwezi kushamiri iwapo wananchi walio wengi si washiriki.”

Mheshimiwa Spika, narudia, “Uchumi wa soko hauwezi kushamiri iwapo wananchi walio wengi si washiriki… Mkakati mmojawapo ambao tayari tunaushughulikia ni wa kutambua rasmi rasilimali na biashara za wanyonge ambazo bado ziko kwenye sekta isiyo rasmi ili zitumike kuwafanya wawe washiriki kamili kwenye uchumi rasmi wa Taifa.” Mwisho mwa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi hii ni yetu sote, sisi wote ni wadau wa maendeleo wa nchi yetu. Haiwezi kufanywa na watu wa nje, tuiwezeshe sekta hii ikue na kushamiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo, tarehe 26 Juni, 2007 wakati nikiwasilisha hotuba yangu ya Bajeti niliiarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeridhia kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo *(Constitutiency Development Fund – CDF).*

Aidha, nilieleza kwamba mchakato wa taratibu za kuanzisha na kusimamia Mfuko huu zinaendelea. Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 7.5 kwa mwaka 2007/2008 ili kugharamia miradi ya wananchi itakayopatiwa fedha kutokana na Mfuko

wa Maendeleo wa Jimbo. Aidha, Serikali inaendelea kukamilisha maandalizi ya Muswada wa Sheria wa Uanzishaji wa Mfuko huo. Taratibu za usimamizi na uendeshaji wa mfuko huu zitafafanuliwa wakati Muswada husika utakapowasilishwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa ufafanuzi wa mambo muhimu kuhusu uanzishaji wa Mfuko huu hasa kwa sababu wapo baadhi ya watu wanaosema kuwa Mfuko maana yake Mbunge anapewa fedha anaweka mfukoni, halafu anaamua mwenyewe anazigawaje. Wengine wamesema pengine Mbunge akipewa anaweza akapeleka nyumbani kwao tu akaacha maeneo mengine. Naomba nifafanue:-

(i) Lengo kuu la Mfuko huu ni kuongeza chachu mpya ya maendeleo katika Jimbo. Hivyo ifahamike tangu mwanzo kuwa lengo la Mfuko huu ni kuchangia katika mipango mbalimbali na rasilimali za kusukuma maendeleo katika Jimbo. Kwa maana hiyo, nasisitiza kuwa fedha za Mfuko zinapaswa zitumike kuchangia miradi ya maendeleo ya wananchi ili kuhamasisha maendeleo katika Jimbo. Taratibu zote za Serikali za uwazi na usimamizi wa fedha zizingatiwe. *(Makofi)*

(ii) Pili, Majimbo yote ya Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yatanufaika na Mfuko huu. Kwa upande wa Tanzania Bara, shughuli za Mfuko zitasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na kwa upande wa Tanzania Visiwani, shughuli za Mfuko zitasimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo itaelekeza taratibu zitakazotumika katika uendeshaji na usimamizi wa Mfuko. *(Makofi)*

(iii) Tatu, miongoni mwa vigezo vitakavyotumika kutenga fedha za Mfuko kwa kila Jimbo ni pamoja na ukubwa, eneo la Jimbo husika, idadi ya watu na kiwango cha umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuwa katika Bajeti ya mwaka wa 2007/2008, katika kutekeleza sera ya kupeleka madaraka kwa wananchi *(D by D)*, Serikali imeelekeza jumla ya shilingi bilioni 286 kwenda kwenye Halmashauri zote nchini. Narudia, tumeelekeza shilingi bilioni 286 kwenda kwenye Halmashauri zote nchini. Kiwango hicho ni wastani wa shilingi bilioni 20 kwa kila Mkoa, hizi ni fedha kwa ajili ya maendeleo. Nasisitiza kuwa shauku ya Waheshimiwa Wabunge katika usimamizi na ufuatiliaji wa fedha za maendeleo kwenye Halmashauri, usije ukajikita zaidi kwenye kusimamia Mfuko wa Jimbo pekee yake. Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha kuwa matumizi ya fedha zitakazopelekwa Wilayani yanasimamiwa vizuri ili zilete tija *(value for money)* yaani *we must go for value for money.* Ni matarajio ya Serikali kuwa fedha zote hizo zilizotengwa zitaongeza kasi ya wananchi kujiletea maendeleo na kuondoa umaskini nchini. *(Makofi)*

Nategemea tutakapokuja hapa mwaka kesho wakati wa Mkutano wa Bajeti tutaelezana mafanikio, haitakuwa ni kulalamika tena kwamba fedha zimetumiwa vibaya, fedha zimefanyaje, itakuwa ni kuelezana mafanikio kwamba tumepiga hatua kiasi gain na nasema bado nasisitiza hili ni jukumu la Mbunge, tumekuja hapa kuzungumza hapa

habari ya maendeleo ya watu sasa tukasimamie hizo fedha zilete maendeleo ambayo tumeyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika hitimisho, narudia kusema tena kwamba hatua tuliyofikia inaonyesha ndege yetu ya kutafuta maisha bora kwa kila Mtanzania imeanza kupaa. Tunayo kila sababu ya kujivunia na kuwaambia wenzetu ambao hawayaoni haya ambayo yametekelezeka kwa kipindi hiki kwamba wafungue macho yao na kuona kilichofanyika, tulichokifanya kinaonekana. Hawa wanaobeza kwamba hatujafanya kitu wajiulize wao wamefanya nini kuisaidia nchi yetu? *(Makofi)*

Narudia tena kusema kwamba hatua tuliyofikia inaonyesha kwamba ndege yetu ya kutafuta maisha bora kwa kila Mtanzania imeanza kupaa. Wapenda dhihaka wataendelea kudhihaki, Wapinzani wataendelea kupinga maana ndiyo kazi yao, lakini kwa jasho la Watanzania na kwa uongozi bora wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Tanzania inasonga mbele, dunia inaona hivyo na dunia inakiri hivyo. Safari bado ni ndefu, lakini kuendekeza mashaka na kebehi si njia ya kufika tunakotaka kwenda na kila mmoja wetu, hata wenye dhihaka na Wapinzani, wanayo sehemu muhimu katika kuifikisha Tanzania inakopasa kuwa yaani penye maisha bora kwa kila Mtanzania. Tunahitaji kupeana matumaini, si kukatishana tamaa hasa pale inapoonekana wazi kuwa matumaini hayo yamejengwa juu ya msingi imara na si ubabaishaji. Narudia, kila kiongozi na kila mwananchi anayo nafasi na wajibu katika kuwaletea Watanzania maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliwahi kusimuliwa hadithi ya Mchungaji mpya aliyepangiwa kuhudumia Kanisa moja kwenye nchi tajiri ambapo watu walikuwa wameacha kabisa kwenda kusali. Akatumia kiasi cha siku nne kuwasihi waliokuwa waumini warejee Kanisani kumsikiliza bila mafanikio. Basi akanunua nafasi kwenye gazeti la eneo lake akaweka tangazo kwenye gazeti kuwaalika waliokuwa waumini wake waje kwenye misa ya wafu kwa ajili ya Kanisa maana lilikuwa limeshakufa. Tangazo hilo likawafanya wananchi wale wawe na hamu kujua misa ya wafu kwa ajili ya Kanisa inakuwaje. Siku ya siku wakajaa Kanisani waone kulikoni. Wakaona jeneza kubwa lililopambwa kwa maua mengi. Baada ya kusoma wasifu wa marehemu kanisa, Mchungaji akawaalika waliokusanyika pale wapite mbele kutoa heshima zao za mwisho. Mstari mrefu ukaanza, lakini kila aliyechungulia ndani ya jeneza aliondoka kwa fedheha na aibu kubwa maana ndani ya jeneza kulikuwa na kioo kikubwa na kila aliyechungulia ndani ya jeneza alijiona mwenyewe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na sisi kadhalika, haiwezekeni kujiweka kando na kudhani matatizo ya nchi hii ni ya Serikali peke yake. Ukweli ni kuwa matatizo yanapotokea ni yetu sote. Tukifanikiwa tumefanikiwa wote, tukishindwa tumeshindwa wote maana hii nchi yetu sote. Hivyo kabla ya kuhitimisha hotuba yangu napenda kusisitiza mambo yafuatayo:-

(a) Tunalo jukumu la kukuza ajira nchini. Nafasi tunazo na hasa kwa kutumia sekta isiyo rasmi. Kama kila mmoja wetu atafanya kazi kwa bidii katika eneo alipo, nchi yetu itapiga hatua ya maendeleo na matokeo yataonekana. *(Makofi)*

(b) Tumejiridhisha kwamba uchumi wetu unakua kwa kasi ambayo tukiiendeleza tutapata mafanikio makubwa. Tuungane pamoja kukuza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

(c) Vijana wetu waliopo shule za msingi na sekondari wanakaribia kufanya mitihani yao. Tuwajengee madarasa mapema kwa wale watakaofaulu kujiunga na kidato cha kwanza na cha tano na nyumba za walimu. *(Makofi)*

(d) Watanzania wote tujitahidi kufanya kazi kwa bidii zaidi na maarifa zaidi na kutumia muda wa kazi kikamilifu tukiwa na lengo la kuboresha maisha yetu. Tunao wajibu na ni jukumu letu kutekeleza kwa bidii yote haya.

(e) Twendeni Waheshimiwa Wabunge tukasimamie utekelezaji wa yale yote yaliyopitishwa na Bunge hili Tukufu. Tuwaongoze wananchi na kuwapa moyo wa kufanya kazi. Tusiwavuruge, bali tuwe dira ya uongozi mzuri ili kufikia malengo yaliyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii tena kukushukuru wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kutuongoza vizuri sana wakati wote wa Mkutano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kikao hiki kilikuwa nafasi ya kukupima uwezo wako wa kuongoza Bunge linapopata matatizo kidogo. Umeonesha una uwezo wa hali ya juu sana. Nakupongeza sana. *(Makofi)*

Nawashukuru Wenyeviti wote wa kudumu kwa kutuongoza vizuri. Niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao pamoja na watumishi wote wa Serikali walioisaidia Serikali kujibu maswali na kuwasilisha hoja za Serikali hapa Bungeni. Namshukuru Katibu wa Bunge Bwana Damian Foka, pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kufanikisha Mkutano huu. *(Makofi)*

Mwisho nawashukuru Waandishi wa Habari kwa kazi nzuri walioifanya ya kuwafikishia habari wananchi kuhusu yanayotokea Bungeni. Wamefanya kazi nzuri, nawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Chama cha Mapinduzi kipo katika mchakato wa uchaguzi katika ngazi za Wilaya na Mikoa. Aidha, maandalizi ya Mkutano Mkuu wa CCM utakaofanyika Dodoma katika eneo la Kizota yanaendelea. Naelewa joto la uchaguzi wa Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa linapanda siku hadi siku. CCM ina mengi ya kufundisha katika eneo hili la uchaguzi. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kuwatakia wote walioteuliwa kuwania nafasi zote za uchaguzi mafanikio na kila mmoja kwa nafasi yake namtakia ushindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu niwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Monduli, wamenivumilia sana. Hata wasiponiona wajue bado nitaendelea kuwahudumia kwa nguvu zangu zote. Nimshukuru sana mke wangu Regina na wanangu kwa kuniunga mkono wakati wote wa kazi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunahitaji ushirikiano wa pamoja, kwa kila mmoja wetu kushiriki katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kufikia malengo ya maendeleo ya nchi yetu. Mwanafalsafa mmoja aliwahi kusema kuwa hesabu ngumu kuliko zote ni hesabu ya baraka na sisi tusipoangalia hesabu hiyo itatushinda. Tuondoke hapa Dodoma tukitambua baraka za nchi yetu na matunda ya kazi iliyofanyika. Nawatakieni safari njema wakati wa kurudi katika vituo vyenu vya kazi na kila mmoja wenu afike salama kwenye jimbo na atupelekee salamu kwa wanajimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi siku ya Jumanne, tarehe 30 Oktoba, 2007 saa 3:00 asubuhi litakapokutana hapa mjini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Nina hakika Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mmefarijika sana na hotuba hii muhimu sana ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ikiwa pia ndiyo hoja ya kuahirisha Bunge. Nimemwandikia *Chief Whip* kwamba kutokana na umuhimu wa yaliyosemwa humo tunaomba utaratibu ufanywe ichapishwe haraka ili kila Mbunge aweze kupata nakala. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, binafsi kwa niaba ya Naibu Spika, Wenyeviti na watumishi wa Ofisi ya Bunge napenda kukushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maneno yako ya kutupa nguvu. Haya mnayoyaona yanayotokea sasa ni rasha rasha tu, tunajua siku za usoni watajitahidi baadhi ya wenzetu kufanya mambo mengine tena lakini napenda niwahakikishie niko imara, nitalilinda, hadhi ya Bunge inalindwa na Katiba na nitaisimamia Katiba kama nilivyoapa na msiwe na wasiwasi hata kidogo juu ya hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyo mbele yetu ni ya kuliahirisha Bunge hadi siku ya Jumanne, tarehe 30 oktoba, 2007 saa tatu asubuhi hapa Dodoma. Hoja hiyo imetolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na imeungwa mkono. Tumefanya utaratibu na Mheshimiwa William Lukuvi wale wasioafiki watabaki hapa hapa bila kwenda majimboni kwao na watahudumiwa na Mkoa wa Dodoma kwa posho za Magereza. *(Makofi)*

Sasa natangaza kuliahirisha Bunge hili hadi siku ya Jumanne, Tarehe 30 Oktoba, 2007 saa tatu kamili asubuhi ndani ya Ukumbi huu hapa Dodoma. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 05.45 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 30 Oktoba, 2007 saa tatu asubuhi)*